**Ukiendesha** gari umelewa kutupwa selo hadi mwakani

UKURASA 3



RIPOTI MAALUM

**Wizi** wa matini janga linalotikisa elimu ya juu

UKURASA 4


Kahama yaja na staili pembejeo bure kwa vijana kukuza kilimo na ajira zao

BUFE

IJUMAA DESEMBA 18, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Tarime yawekeza uchumi katika majengo yatakayoingiza mamilioni kodi, ajira kibao

Umaskini unavyopigwa deki Kibaha kupitia msaada sheria

• Kinara watoto wanaotelekezwa

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Desemba 18, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580433

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wakurugenzi matatani kwa ununuzi wa magari

• **Waziri** Mkuu aibua tuhuma ufisadi ujenzi stendi ya mabasi na malori... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**MHANDISI KORTINI TUHUMA UDANGANYIFU**

MKUU wa Idara ya Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Mhandisi Mathias Shoto (38) na Msaidizi wake...

UKURASA WA 19

**RWANDA YARIDHISHWA UTENDAJI BANDARI DAR**

RWANDA imeeleza kuridhishwa na huduma zinazotolewa katika Bandari ya Dar es Salaam, ambayo inahudumia...


## Kikwete aongoza mazishi ya Subhash

UKURASA 3



Wafanyakazi wa kampuni za Motisun wakitoa heshima zao za mwisho mbele ya jeneza la Mwenyekiti Mtendaji wa makampuni hayo, Subhash Patel, katika eneo la viwanda vyake Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


# Maelfu wakosa sekondari kwa ukosefu wa madarasa

UKURASA 2


**MICHEZO** SVEN AKUNWA NA KMC, AIFUNGIA KAZI PLATINUM UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wakosa nafasi sekondari kwa ukosefu wa madarasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI 74,166, sawa na asilimia 8.9 ya waliofaulu mtihani wa taifa wa darasa la VII mwaka huu, hawajapangiwa shule katika awamu ya kwanza kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwakani kutokana na uhaba wa madarasa.

Kati yao, wavulana 34,861 na wasichana 39,305.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alibainisha hayo jana, alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwakani.

Alisema kutokana na hali hiyo, anawataka wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na wa mikoa kuhakikisha wanasimamia kwa karibu ujenzi wa vyumba vya madarasa ili ukamilike kabla ya Februari 28 mwakani.

"Mwaka huu kama nilivyosema kuwa tunataka kila mtoto mwenye sifa ajiunge na kidato cha kwanza bila kukosa, hivyo niwatake watendaji katika ngazi mbalimbali kuhakikisha ujenzi wa madarasa kwa ajili ya watoto hawa unakamilika kwa wakati," aliagiza.

Jafo alisema mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 1,480 ambavyo vinatakiwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao waliokosa nafasi katika awamu hiyo ya kwanza.

"Nimefanya ziara katika maeneo mbalimbali limekuta ujenzi unaendelea kwa kasi na sehemu nyingi walichelewa kutokana na kile kipindi ambacho saruji iliadimika, lakini tunashukuru serikali kuingilia kati hivi sasa saruji ipo na ifikapo Februari 28 mwakani, wanafunzi wote watajiunga na masomo yao ya kidato cha kwanza," alisema.

Aliitaja mikoa na idadi ya wanafunzi waliobaki ambao watapangiwa shule katika awamu ya pili kadri mikoa na halmashauri zitakavyoendelea kukamilisha ujenzi vyumba vya madarasa na madawati.

Mikoa hiyo ni Arusha (2,768), Dar es Salaam (14,926), Dodoma (7,145), Geita (9572), Iringa (907), Kigoma (5,549), Kilimanjaro (3,015), Manyara (557), Mara (7,809), Mbeya (5,549), Pwani (6,888), Morogoro (4,686), Rukwa (564), Shinyanga (234), Simiyu (1,837), Singida (674) na Tanga (1,537).

Alisema mwaka huu wanafunzi 1,008,307 walifanya mtihani huo wa kuhitimu elimu ya msingi kukiwa na ongezeko kulinganisha na wanafunzi 933,077 wa mwaka 2019.

Kati yao, waliofaulu na kuwa na sifa za kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza ni 759,737, sawa na asilimia 81.42 ya waliofanya mtihani huo.

Jafo alisema katika awamu hii ya kwanza jumla ya wanafunzi 759,706, sawa na asilimia 91.1 ya wanafunzi waliofaulu wakiwamo wavulana 368,174 na wasichana 391,532 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Alisema kati ya waliochaguliwa, wanafunzi 4,169 wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni.

"Wanafunzi 970 watajiunga na shule za wanafunzi wenye ufaulu mzuri, wanafunzi 1,238 watajiunga na shule za ufundi, wanafunzi 1,961 watajiunga na shule za bweni za kawaida," alisema.

Jafo alisema wanafunzi 755,537 wakiwamo wavulana 362,247 na wasichana 385,665, wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za kutwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kuwa miongoni mwa waliochaguliwa, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni 2,491 wakiwamo wavulana 1,312 na wasichana 1,179, sawa na asilimia 75 ya wanafunzi wenye ulemavu waliofanya mtihani huo.

"Jumla ya mikoa tisa ambayo ni Kagera, Katavi, Lindi, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Songwe na Tabora imewapangia shule wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021," alisema.

Alisema kuwa mwaka huu kwa mara ya kwanza uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza umefanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Alisema faida za mfumo huo ni pamoja na kupunguza muda mwingi uliokuwa ukitumika kuchagua wanafunzi wa kidato cha kwanza katika ngazi ya mikoa na kuongeza ufanisi.

"Ninawahimiza wazazi, walezi na jamii kushirikiana na uogozi wa wilaya, halmashauri na shule kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kubaki shuleni hadi watakapohitimu elimu ya sekondari," aliagiza.



Mkuu wa Kikosi cha Polisi, Usalama Barabarani Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Nuru Seleman (wapili kushoto), akikabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo ya usalama barabarani kwa mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Turiani, Maria Mahajile, wakati wa ufunguzi wa mradi wa elimu ya usalama barabarani kwa vijana wadogo na madereva bodaboda Tanzania, unaoendeshwa na Shirika la Amend na Total Foundation, shuleni hapo jijini Dares Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Jean Francois Schoepp. **PICHA: JOHN BADI**

# Wakurugenzi watatu matatani ununuzi magari

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZIARA ya siku mbili ya Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa jijini Mwanza, imeibua 'madudu' kwa halmashauri tatu za mikoa ya Shinyanga na Mwanza, akiwapa siku saba wakurugenzi wake kujieleza kwanini wamenunua magari ya kifahari.

Vilevile, Majaliwa amezishukia Halmashauri za Jiji la Mwanza na Ilemela kwa mwenendo mbovu katika ukusanyaji wa mapato kwa mwaka huu wa fedha.

Wakurugenzi waliotakiwa kujieleza ni wa Jiji la Mwanza, Msalala na Kahama, huku Majaliwa akimtaja Mkurugezni wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Kilomoni Kibamba, kujieleza kwa kununua gari la kifahari lenye thamani ya Sh. milioni 270 ilhali ameshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Maagizo hayo aliyatoa jana jijini Mwanza, muda mfupi baada ya kuwasili kwa ziara yake ya siku mbili na kuzungumza na watendaji wa serikali katika kikao kazi.

Wakati wa kikao hicho, Majaliwa alimsimamisha Kibamba na kumtaka atoe maelezo kuhusu ununuzi wa gari hilo, ndipo mkurugenzi huyo alipobainisha kwamba alitumia Sh. milioni 270, lakini kwa Halmashauri za Msalala na Kahama haikutajwa thamani ya magari ya kifahari yaliyonunuliwa.

Majaliwa alisema anashangaa wakurugenzi wa halmashauri hizo tatu kununua magari ya kifahari huku kukiwa na shida nyingi zinazowakabili wananchi.

Kuhusu makusanyo ya mapato, Majaliwa alisema Halmashauri ya Jiji la Mwanza imekusanya kwa asilimia 39 na Ilemela kwa asilimia 35, kiwango ambacho ni kidogo.

Waziri Mkuu alisema kuwa kufikia sasa, halmashauri hizo zilitakiwa ziwe zimekusanya mapato kwa asilimia 50, lakini zimeshindwa kufikia malengo ya mwaka huu wa fedha.

"Makusanyo kwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ni asilimia 39 na Ilemela ni asilimia 35 kwa nusu mwaka wa fedha 2020/21, walitakiwa wafikie asilimia 50, halafu mtu ananunua gari la kifahari, ni matumizi mabaya ya fedha," Majaliwa alionya.

Kiongozi huyo wa serikali pia alihoji gharama za mradi wa kituo cha mabasi na malori uliopo eneo la Nyamohongoro wilayani Ilemela baada ya kubaini gharama zake ni za juu wakati kulikuwapo na mzabuni wa gharama nafuu.

Alisema mradi huo ambao kwa sasa unajengwa kwa gharama za Sh. bilioni 22, ulikuwa na uwezekano wa kujengwa chini ya kiasi hicho cha fedha.

Majaliwa alisema Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ilemela, alishauriwa kutumia mkandarasi wa bei ya chini, lakini akakataa na hivyo kuamua kujenga kwa gharama hiyo.

Aliongeza kuwa kutokana na mtafaruku huo, mkurugenzi huyo amejenga chuki na mtaalamu wa uchumi wa halmashauri hiyo na kuamua kutompandisha cheo kwa takribani miaka miwili sasa.

Kwa kutambua suala hilo, Majaliwa alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emanuel Tutuba, kumpandisha cheo mchumi huyo wa halmashauri baada ya kukaimu nafasi hiyo kwa miaka miwili.

Katika ziara hiyo, Majaliwa pia alipata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi na malori kilichoko Nyamhongoro wilayani Ilemela.

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuweka mpango mkakati wa mwaka 2020/21, ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuendana na kasi ya maendeleo ya serikali ya awamu ya tano.

# JK aongoza maelfu kumzika Subhash

**Na Halfani Chusi**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, jana aliongoza maelfu ya watu katika maziko ya mwili wa mfanyabiashara Subhash Patel, jijini Dar es Salaam.

Maziko hayo yalifanyika Kijitonyama jijini yakihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.

Naibu waziri huyo alisema Patel ameacha pengo kubwa katika taifa, akisifu uzalendo alikuwa nao kwa nchi.

"Patel alikuwa ni mpambanaji na mzalendo wa taifa letu, alitufanya tujue kuwa hata Tanzania tunaweza kuwa na viwanda kupitia rasilimali zetu, alikuwa ni mmoja kati ya watu waliosaidia nchi kufikia uchumi wa kati maana alijenga viwanja vingi na alifanikiwa kuajiri watu wengi na wengi wao ni Watanzania," alisifu.

Aliongeza kuwa serikali ya awamu ya tano inajipambanua kuwa ni serikali ya viwanda, hivyo watendaji wake wataendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wajasiriamali ili kujikwamua kiuchumi kupitia viwanda.

Alibainisha kuwa Patel aliyefariki dunia mwanzoni mwa wiki, ameacha viwanda 15.

Mfanyabiashara huyo alikuwa kwenye mchakato wa kuanzisha kiwanda cha makaa ya mawe Ludewa, kiwanda cha saruji Mamba, Bagamoyo na kiwanda cha Sayona - Mbeya.

# Ukiendesha gari umelewa kutupwa 'selo' hadi mwakani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani mwake kuwakamata madereva walevi na kuwaweka lupango hadi sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya zitakapopita. Lengo la kiongozi huyo ni kupunguza ajali na kulinda uhai wa wananchi.

Alitoa agizo hilo wakati wa maadhimisho ya kilele cha siku 16 za kupinga ukatili na unyanyasaji wa kijinsia yaliyoadhimishwa Viwanja vya Ofisi ya Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Arusha na Mtandao wa Polisi Wanawake Mkoa huo (TPF NET).

Alisema kumekuwa kujitokeza ajali zisizo za lazima kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka, zinazosababishwa na madereva wazembe wasiotaka kufuata sheria za nchi kwa kunywa pombe kupita kiasi kisha kuendesha vyombo vya moto.

"Sasa hapa mkoani kwangu sitaki ajali za makusudi kuanzia sasa, RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) ninakuagia, ukikuta mtu amelewa huku anaendesha chombo cha usafiri, kamata weka ndani mpaka sikukuu zote hizi zipite, ninajua wataongea sana sababu dhamana ya haki ni ya kila mmoja, lakini uhai wa kila mtu ni mali ya serikali, hivyo lazima tuulinde kwa kukuhifadhi ndani," aliagiza Kimanta.

Alisema kumekuwa na tabia ya watu kukamatwa na kuwekwa lupango kisha baada ya siku moja au siku hiyo hiyo, wanapewa dhamana, akisisitiza "tabia hiyo ikome".

Kimanta alisema madhara yanayosababishwa na madereva walevi ni makubwa kuliko wao kusaidiwa kuhifadhiwa ndani.

Aliwaomba wananchi kuchukua tahadhali ya kutoacha nyumba zao bila watu katika kipindi hiki kuelekea sikukuu hizo mbili.

"Hivi sasa wahalifu wamebadili mfumo, wanavunja nyumba mchana na kuiba badala ya usiku kwa sababu ya doria za polisi zinatisha, sasa nanyi wananchi hakikisheni mnaweka watu nyumbani, msitoke wote, japo polisi wataongeza doria mchana na usiku ila nanyi chukueni tahadhali," alishauri.

Kimanta alisema ingawa Jeshi la Polisi limejitahidi kulinda maeneo yote, kila mtu anapaswa asimame katika nafasi yake na kufichua wahalifu anaowafahamu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salumu Hamduni, alisema amepokea maelekezo ya mkuu huyo na atayafanyia kazi, ili kila mmoja aheshimu sheria za barabarani na sikukuu zipite kwa usalama bila ajali mkoani humo.

# Mbunge ahimiza ukusanyaji mapato

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

MBUNGE wa Ludewa, Joseph Kamonga, amewataka madiwani kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani, ili kuboresha afya, elimu na miundombinu.

Pia amewataka madiwani kushirikiana na wataalamu wa halmashauri hiyo, ili kufikia malengo ya kuwakomboa wananchi kiuchumi kupitia sekta hizo.

Kamonga aliyasema hayo juzi baada ya hafla ya kuwaapisha madiwani iliyofanyika katika ukumbi wa halmashauri na kuwataka kutokusubiri serikali itumie nguvu katika kufanikisha hilo.

"Wakuu wa idara mimi ni mtaalamu mwenzenu, nimekuwa kwenye utumishi wa halmashauri kwa muda mrefu. Ninaomba tushirikiane katika ukusanyanyi wa mapato," alisema. "Tusipohangaika kukusanya mapato, tutashindwa kutatua changamoto za wananchi, tuendelee kuhamasishana tukiamini jukumu la kuleta maendeleo ni letu sote," aliongeza.

Hata hivyo, alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Sunday Deogratius, kwa kuendelea kukuza kiwango cha ukusanyaji wa mapato.

"Mwaka wa kwanza aliofika, mkurugenzi alikusanya Sh. milioni 600, mwaka uliofuata alikusanya Sh. milioni 800 na mwaka huu amesema ana mpango wa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni moja na mpaka sasa ameshafikisha asilimia 55," alisema.

Pia alisema katika suala la usafiri kwenye Ziwa Nyasa kutokana na kusimamishwa, ataendelea kufuatilia ili kujua zaidi undani wa jambo huilo. "Kule Ziwa Nyasa tunashukuru Rais alitutengenezea meli tatu, lakini meli zile zilifanya safari moja halafu zikapaki. Tunaendelea kufuatilia kuhakikisha wananchi waliotuchagua hatuwaangushi," alisema Kamonga. Diwani wa Mlangali, Hamis Kayombo (CCM), alisema wameyapokea yote waliyoaswa ikiwamo suala la mapato ambalo ndio msingi wa halmashauri.


IITA
Transforming African Agriculture

IRRI

## POSITION ANNOUNCEMENT

**Researcher – Agronomy**

**IITA-TZ-2020 - IRRI-005 -NRS-MOROGORO**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Researcher – Agronomy**

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium. We develop new rice varieties and rice crop management techniques that help rice farmers improve the yield and quality of their rice in an environmentally sustainable way. We work with our public and private sector partners in national Agricultural research and extension systems in major rice growing countries to do research, training and knowledge transfer.

**A Researcher – Agronomy** will facilitate the planning, designing and implementation of the routine trials, data collection and analysis, and other research activities of projects on Rice production improvement and responses to abiotic stresses in Tanzania focusing on the development of improved rice varieties, production systems and post-harvest technologies and on training farmers, technicians and extension officers will constantly communicate with internal and external project partners and collaborators to exchange conceptual ideas and to effectively gather feedback and research-related requirements for the advancement of the projects. Consolidate, evaluate and analyze research data gathered from trials, and draft reports and presentations.

**Duty Station: The position will be based Morogoro, Tanzania.**
**Criteria for Success / Qualifications**
MSc in Agriculture with minimum 2 years post graduate work experience from which at least 1 year in rice research/development.

**Skills and knowledge**
**mandatory**
- Has proven technical proficiency in conducing research experiments and field trials
- Has strong experience in field management (layout, irrigation, fertilization, pest and disease monitoring)
- Has experience in statistical analysis and report preparation
- Has strong oral and written communication skills
- Has strong analytical skills

**Preferred**
- Has strong technical experience in guiding farmers, technicians and extension officers
- Has experience in phenotyping and assessing rice responses to different abiotic stresses

**Responsibilities**
**3.1. Purpose**
- Undertake and supervise phenotyping of rice germplasm under different abiotic stresses, both in controlled environment facilities and in the field
- Facilitate the planning, designing and implementation of the routine trials, data analysis and other research activities of projects on rice crop improvement in Tanzania focusing on the development of improved climate resilient varieties, production systems and on training farmers, technicians and extension officers.
- Contribute to the development of the research projects including selection of adequate research tools and equipment, verification of suggested methodologies and establishment of parameters related to rice production intensification
- Oversee maintenance of the research areas, research fields, technical equipment and fields staff

**3.2. Engagement**
- Constantly communicate with internal and external project partners and collaborators to exchange conceptual ideas and to effectively gather feedback and research-related requirements for the advancement of the projects
- Provide assistance and guidelines to internal and external stakeholders considering efficient implementation of the projects
- Constantly monitor, evaluate and provide recommendations to improve research and training activities/tasks performed by Research Technicians and contract workers in order to maintain smooth conduct of field and greenhouse trials as well as to foster a productive working environment
- Coordinate with required IRRI services and supplies and with project partners from Sokoine University of Agriculture and University of Copenhagen, to ensure smooth implantation of experiments and proper data collection, analyses and reporting

**3.3. Delivery**
- Consolidate, evaluate and analyze research data gathered from the project trials
- Evaluate, validate and contribute to the interpretation of results, contribute to the writing of manuscripts for reports/publications as well as presentations/posters for national and international conferences
- Prepare and submit updated research outputs to the Scientist II - Plant Breeding in a timely manner
- Supervise and lead the maintenance of accurate data recording and updating of database for efficient storage and retrieval of information

**General information:**
The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date: Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.**
**Please note that only shortlisted candidates will be contacted.**

RIPOTI MAALUM

# Wizi wa matini; janga linalotikisa vyuo vikuu

## ■Maprofesa wafichua 'madudu' yaliyopo
## ■Kilio: Shahada za kufanyiwa, elimu butu

Na Sanula Athanas

HIVI sasa kuna kilio cha ubabaishaji katika kufanikisha maandiko ya kitaaluma vyuoni, ambacho zaidi kinasikika katika ngazi za uzamili na uzamivu.

Maandiko ya utafiti wa kitaaluma yanalalamikiwa kutofikia viwango stahiki na kusababisha kupotea kwa sifa sahihi anazopaswa kuwa nazo mhitimu.

Hapo ndipo panapozua maswali -- kwanini zama zilizopita ambazo pia hazikuwa na maendeleo makubwa kiteknolojia na mengine yanayofanana nayo, ufanisi ulikuwa juu na sasa unaanguka?

Kimsingi, wajibu mkuu wa taasisi yoyote ya elimu ya juu, vikiwamo vyuo vikuu, ni kufundisha, kutoa ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti.

Profesa Mugyabuso Mulokozi, mwanazuoni mstaafu na mbobezi katika Kiswahili, anayataja maandiko hayo tajwa ya kitaaluma kwa jina la 'matini'.

Mkongwe huyo wa iliyokuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), anaitafsiri matini kuwa ni kazi ya uandishi iliyowekwa katika machapisho ya kitaaluma.

Vilevile, Kamusi ya Oxford (2000) inaibebesha matini maana ya wazo au mfululizo wa mawazo unaojitosheleza kimaana, huku Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) ikiifasili kuwa ni kifungu cha habari kilichoandikwa.

Ndani ya uelewa wa maana hiyo, ndipo Nipashe ilipojielekeza kutafuta majibu kwa wanazuoni wanaohudumia ngazi hiyo ya elimu, kupata siri ya uharibifu unaolalamikiwa.

Wasomi hao wanatoa ufafanuzi na kuanika uzoefu na ushuhuda wao kuhusu viashiria hivyo vya janga kwa elimu nchini na ukakasi unaojitokeza katika kitaaluma.

Dk. Newton Kyando, Mhadhiri Mwandamizi katika Kitivo cha Elimu cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), anasema udanganyifu katika matini unatokana na uvivu, uzembe na tamaa ya kuhitimu, ili kupanda madaraja na faida zake pasi na kutoka jasho la kitaaluma.

Mwanazuoni huyo pia ana angalizo kwamba kadhia hiyo ni zao la mifumo dhaifu ya elimu na uendeshaji wake katika nchi zinazoendelea pamoja na walakini katika stadi za lugha ya kufundishia.

"Wapo wanafunzi ambao wanafanya wizi wa maandishi ya kitaaluma kwa sababu hawaelewi lugha inayotumika kufundishia katika kuelezea dhana fulani, hivyo kujikuta wameingia kwenye wizi," Dk. Kyando anabainisha.

Anafafanua uzoefu wake kwamba ameshakutana na wanafunzi ambao ni mahiri kutetea hoja kwa Kiswahili, lakini kinageuka kuwa kitendawili wanapohamia kwenye lugha ya Kiingereza.

Hivyo, anasema mbadala ambao hujitokeza na siyo halali kitaaluma, wanachukua maandiko ya Kiingereza ya wasomi wengine wenye umahiri, kujaza mapengo ya walikokwamia wao, kukidhi mahitaji ya dhana husika.

Mwanazuoni huyo anayataja madhara yatokanayo na vitendo hivyo yanajumuisha kupata wahitimu wasiokidhi vigezo na ubora wa soko katika sekta ya umma na binafsi.

"Wizi wa maandishi ni tatizo linalorudisha nyuma maendeleo ya sekta ya elimu hususani katika maandalizi ya wataalamu wenye weledi kwenye taaluma mbalimbali kitaifa na kimataifa," Dk. Kyando anaonya.

**MBINU KUBAINI WIZI**

Profesa Mulokozi anatumia umahiri wake kubainisha namna wanavyotambua anachokiita wizi wa maandishi katika matini, machapisho na tasnifu.

Anagusia stadi zao ni pamoja na kutathmini kilichoandikwa kwenye kurasa za mwanzo za tasnifu na kuzilinganisha na mtiririko wa kurasa za ndani kupata uwiano.

"Kutokana na ukweli kuwa Watanzania wengi siyo mahiri wa Kiingereza, mara nyingi kurasa za mwanzo za tasnifu zinakuwa na matatizo kwa sababu huandikwa na mwanafunzi mwenyewe.

"Mhadhiri akiwa makini katika eneo hili, inamsaidia kugundua wizi wa maandishi kirahisi akilinganisha na kurasa za ndani kwa kuangalia aina ya lugha katika sehemu hizo," Profesa Mulokozi anasema.

Katika kudhibiti wizi huo wa matini, Profesa Mulokozi anasema watahini wa ndani na wa nje wanapaswa kutekeleza kikamilifu majukumu yao ili kupata kazi bora za kitaaluma.

Anasema pamoja na uwapo wa teknolojia tumizi zinazosaidia katika ugunduzi wa wizi wa maandishi, bado kuna tatizo kwa tasnifu zinazofanyika kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa lugha hiyo haijaingizwa kwenye mfumo hiyo ya kidigitali.

Mhadhiri katika Kitivo cha Usimamizi wa Biashara cha OUT, Proaches Ngatuni, anasema pamoja na matumizi ya teknolojia, wanafunzi wana uwezo wa kutumia programu tumizi ambazo zinawapa mwanya kukwepa kugundulika kufanya makosa ya wizi wa matini.

Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kimeanzisha utaratibu kinaoamini hautoi fursa kwa mwanafunzi kufanya udanganyifu katika kuandika ripoti ya utafiti.

Profesa Ally Namangaya wa chuo hicho anabainisha hatua wanazochukua zinajumuisha mwanafunzi kupangiwa mada ya kufanyia utafiti.

"Akishamaliza kuandika ripoti yake, tunaingiza kwenye programu maalum inayotambua kiwango cha udanganyifu. Kama kitazidi asilimia 25, basi kazi hiyo inatupwa," anasema.

Mkuu wa Kitivo cha Sheria cha OUT, Dk. Rindstone Ezekiel, anasema kukithiri kwa wizi wa maandishi kunatokana na majukumu mengi waliyonayo wahadhiri, hivyo kukosa muda wa kupitia kazi hizo kwa umakini.

"Shida nyingine ni kuwapo kwa wanataaluma ambao wanaridhika kwa kuangalia tu kazi kwa juu juu na mwonekano wa nje," Dk. Ezekiel analalamika.

Msomi huyo anafichua baa lingine kwamba katika taasisi nyingi za elimu ya juu, wapo watu ambao wanasaidia wanafunzi kuandika utafiti na tasnifu na ofisi zao ziko maeneo jirani na vyuo.

Anasema watu hao huwafanyia wanafunzi utafiti na malipo ya maelewano yao mara nyingi huhusisha fedha, hivyo kuwa sehemu ya wazalishaji wa shahada za kununua.

**NINI KIFANYIKE?**

Mhadhiri Msaidizi wa UDSM, Zamda Geuza, anasema wizi wa maandishi ya kitaaluma utadhibitiwa ikiwa wadau wote wataheshimu maadili ya kazi na kutimiza wajibu wao.

"Tatizo hili litakomeshwa ikiwa tu pande zote kwa maana ya mwanafunzi na mtahini wa ndani na nje wakizingatia maadili ya kazi na kutimiza wajibu wao," anasema.

Mhitimu wa Shahada ya Uzamili katika Mawasiliano kwa Umma, Vincent Mpepo, anakiri kwamba tatizo la wizi wa kazi za kitaaluma lipo na ni kubwa nchini.

"Lipo kwa ngazi zote za elimu ya juu kuanzia shahada ya kwanza mpaka shahada za ubobevu hususani kwenye utafiti wa kuhitimu ngazi hizo, maarufu tasnifu," anabainisha.

Mpepo anasimulia uzoefu wake binafsi akiwa mwanafunzi wa UDSM akifafanua kwamba:

"Mazingira ya usomaji na ufundishaji huchangia kutokana na baadhi ya watu kuwa wavivu kujisomea vitabu na kupenda urahisi wa kuchukua taarifa kwenye mitandao na vyanzo vingine vya kidijitali.

"Wengi hutamani kuhitimu ili kufanikisha matakwa yao binafsi, yaani waajiriwe au kutetea nafasi za kazi walizonazo."

Mpepo ambaye kwa sasa ni Ofisa Mitihani Msaidizi katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii cha OUT, anasema kadhia hiyo itadhibitiwa ikiwa vyuo vitakuwa na programu tumizi kugundua kiasi cha wizi katika kazi za wanafunzi japo wapo wanaoweza kukwepa kugundulika.

"Kwa wanafunzi, ni muhimu kufuata maadili ikiwamo kutoiba kazi za waandishi wengine, watumie mbinu za kitaaluma zinazokubalika kwa kukiri na kuonyesha kuwa wao siyo wenye mawazo husika ila wamechukua kwa wengine.

"Pia, ni muhimu kufundisha tangu ngazi za chini maarifa ya usomaji, uandishi na hata namna ya kufupisha taarifa wazipatazo wasomaji kutoka vitabuni, mitandaoni na hata kwenye vyanzo vingine," Mpepo anashauri.

Mtazamo huo wa Mpepo unaungwa mkono na Mhadhiri Msaidizi katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya UDSM, Theodora Theodory, anayeshauri kila chuo kiwe na programu tumizi ya kubaini udanganyifu katika matini.

"Udanganyifu wa aina hii una madhara makubwa katika uandaaji wa wataalamu. Kuna wanafunzi wanalazimika kurudia mwaka na wengine kufukuzwa chuo wanapogundulika kujihusisha na udanganyifu huo.

"Kikubwa, ninafikiri ipo haja kila chuo kiwe na vifaa na programu za kubaini udanganyifu huo na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika," Theodora anashauri.



Profesa Mugyabuso Mulokozi.

# Mhandisi kortini tuhuma udanganyifu

**Na Jocktan Ngelly,** GEITA

MKUU wa Idara ya Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Mhandisi Mathias Shoto (38) na Msaidizi wake Hamisi Chande (60), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita.

Shoto na mwenzake wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri kinyume cha kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Walifikishwa hapo mahakamani jana majira ya saa 3:00 asubuhi na kupandishwa kizimbani saa 5:00 asubuhi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Obadia Bwegoge.

Baada ya kusomewa mashtaka yanayowakabili, walikana kuhusika na tuhuma hizo na wako nje kwa dhamana ya mdhamini mmoja kwa kila mshtakiwa mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri, mwenye mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 10.

Wakili Kiongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea maelezo ya awali.

Hakimu Bwegoge alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hadi Januari 13, mwakani.

Akisoma hati ya mashtaka, Murusuri alidai kuwa kati ya Septemba 21, 2012 katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, washtakiwa hao wakiwa wahandisi wa halmashauri, walidai kwamba ujenzi wa daraja la Kakora umekamilika vizuri kama unavyohitajika na fedha zilipwe wakati wakijuwa ni uongo na daraja halijakamilika.

Murusuri alidai kuwa katika shtaka la pili, Juni 7, 2012 katika Halmashauri ya Wilaya, washtakiwa kwa pamoja walitumia nyaraka za kihandisi kwa kumdanganya mwajiri kwamba daraja limekamilika kwa mujibu wa nyaraka za kihandisi wakati siyo kweli.

# Mwambe azikalia kooni taasisi za wizara zake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, ametoa siku saba kwa taasisi zilizo chini ya wizara hiyo, kuwasilisha ukomo wa bajeti na mikakati ziliyojiwekea ili kuleta mabadiliko kwenye sekta za viwanda na biashara.

Pia amewaonya baadhi ya watumishi wa taasisi na wizara kuacha kuwa kikwazo na kuchelewesha huduma kwa wafanyabiashara.

Waziri Mwambe alitoa maagizo hayo jijini hapa alipokutana na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara yake, wakuu wa idara na wafanyakazi wa wizara hiyo.

Alisema kila taasisi ihakikishe imeweka mikakati mipya ya kuleta mabadiliko katika sekta hizo huku akiagiza wakuu hao kutengeneza taarifa za mawasilisho ya majukumu watakayoyafanya kwenye mwaka wa fedha 2020/21.

"Ndani ya siku saba kila taasisi itengeneze taarifa na iwasilishwe kwangu juu ya mikakati mikubwa ya kufanya kazi na kuleta mabadiliko makubwa, kama wewe BRELA (Wakala wa Majina na Leseni za Biashara) tuletee mikakati yako umepanga kufanya nini," alisema.

Alitaka kila kitengo katika wizara kujitafakari wanafanyaje kazi na wamejipangaje katika kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ili kuimarisha sekta za viwanda na biashara zinufaishe taifa.

Sambamba na hayo, aliwataka watumishi kuwa wabunifu katika nafasi zao za kazi na kutengeneza kitu cha tofauti katika utumishi wao utakaoleta mabadiliko chanya katika sekta hizo nchini.

"Tengenezeni mifumo mipya ya utafutaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ili bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini zipate masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema.

"Tuanze kutafuta masoko ya bidhaa zetu. Kuna wajasiriamali wanatengeneza bidhaa lakini hawana masoko. Hawa tunawakatisha tamaa, lakini akizalisha bidhaa na akapata soko inampa nguvu kuendelea kuzalisha zaidi.

"Tuwe wabunifu kuna kiwanda nilikitembelea kinazalisha maziwa lakini vifungashio wanafuata Kenya. Namuuliza anasema hapa nchini hukuna, nikapita kiwanda kingine wanatengeneza vifungashio vile vile naye anasema hana soko hapa tunafanya uzembe hatuwaunganishi hawa wazalishaji," alisisitiza.

Alisema kwa sasa kuna masoko makubwa ya nchini ya bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinapatikana nchini kwa wingi, hivyo ni wajibu wa taasisi zinazohusika kuhamasisha wananchi kuzalisha bidhaa hizo na kutafuta masoko hayo.

Waziri Mwambe aliwataka kutokuwa kikwazo cha kuchelewesha majibu ya maombi ya wafanyabiashara wanapotaka huduma katika ofisi hizo.

"Unakuta mtumishi wa TBS (Shirika la Viwango Tanzania) anashirikiana na mshindani wa mwomba vibali huyu kila akileta maombi ya kuthibitishwa anaambiwa hajakidhi viwango kumbe wewe unazunguka upande wa pili unachukua fedha," alisema Waziri Mwambe.


The Guardian www.ippmedia.com

Nipashe www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII




For our Advertisement Customers

| Just pay for your Print advertisement | Get Free | | | |
|---|---|---|---|---|
| Size of Advertisement | Free E-Paper for One Month | | Free Social Media Post | |
| | The Guardian | Nipashe | Guardian or Nipashe | Guardian or Nipashe |
| Full Page | 10 E-Papers | 10 E- papers | 5 Posts | 5 Posts |
| 3/4 Page | 7 E- Papers | 7 E - Papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 1/2 Page | 5 E- Papers | 5 E- papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 3/8 Page | 3 E- Papers | 3 E- Papers | 1 Post | 1 Post |
| 1/4 Page | 2 E- Papers | 2 E- Papers | 1 Post | 1 Post |



*For More Information Please Contact us:*

0782 253 676 advertise@guardian.co.tz

1. This offer is Valid till 31st Dec 2020
2. Terms and conditions apply

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa nini madarasa yakoseshe watoto kidato cha kwanza?

**TAARIFA** kuwa wanafunzi 74,166, sawa na asilimia 8.9 ya waliofaulu mtihani wa taifa wa darasa la VII mwaka huu, hawajapangiwa shule katika awamu ya kwanza kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwakani kutokana na uhaba wa madarasa, ni za kusikitisha.

Ni masikitiko, lakini ndio ukweli, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Selemani Jafo, alipotoa taarifa hiyo jana jijini Dodoma na kufafanua kuwa kati yao, wavulana ni 34,861 na wasichana ni 39,305.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na wa mikoa kuhakikisha wanasimamia kwa karibu ujenzi wa vyumba vya madarasa ili ukamilike kabla ya Februari 28, mwakani.

Jafo alisema mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 1,480 ambavyo vinatakiwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao waliokosa nafasi katika awamu ya kwanza.

Jafo alisema amefanya ziara katika maeneo mbalimbali na kukuta ujenzi unaendelea kwa kasi na sehemu nyingi walichelewa kutokana na kipindi ambacho saruji iliadimika, lakini baada ya serikali kuingilia kati, kwa sasa saruji ipo na ifikapo Februari 28 mwakani, wanafunzi wote watajiunga na masomo yao ya kidato cha kwanza.

Kwamba wanafunzi waliokosa nafasi awamu ya kwanza watapangiwa shule katika awamu ya pili kadri mikoa na halmashauri zitakavyoendelea kukamilisha ujenzi vyumba vya madarasa na madawati.

Licha ya hatua alizozitangaza Waziri Jafo, kwa upande wetu tunaona kuwa suala la wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tano kuchelewa kujiunga na shule wanazopangiwa kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa na madawati limekuwa likijirudia kila mwaka.

Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa inatokana na kutokuwapo kwa maandalizi ya mapema ya kuwapo kwa miundombinu hiyo wakati kila mwaka idadi ya wanafunzi wa kujiunga na vidato hivyo inakuwa inajulikana mapema.

Suala zina la waliofaulu kukosa madarasa au madawati, hivyo kuchelewa kupangiwa nafasi awamu ya pili lina athari kadhaa kwao na kwa Taifa.

Mosi, wanaweza kujikuta wanakosa kujiamini katika masomo kutokana na kupelekwa haraka ili kuwafikia walioanza kusoma awamu ya kwanza.

Pili, ujenzi wa miundombimu hususan madarasa unapofanyika kwa mtindo wa zimamoto (haraka bila maandalizi ya kutosha) unaweza kutofikia viwango kutokana na kulipua, hivyo baada ya muda mfupi kukuta majengo hayo yanakosa uimara.

Wanafunzi 74,166 waliokosa nafasi awamu ya kwanza kutokana na uhaba wa madarasa ni wengi sana, hivyo tunaishauri serikali kuandaa mkakati maalum ambao utakuwa endelevu katika kulitafutia tatizo hili ufumbuzi.


Kwa mtazamo wetu, serikali hainabudi kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha wadau katika kuchangia kwa njia mbalimbali, zikiwamo harambee kwa ajili ya ujenzi wa vyimba vya madarasa.

Tunasema hivyo tukiwa na uhakika kwamba wadau wengi wataguswa kusaidia kwa kuwa suala la elimu ya watoto linamgusa kila mmoja. Hii inathibitishwa na jinsi wadau walivyojitoa kuchangia madawati baada ya serikali kuanzisha na kuratibu mchakato huo.

Vilevile, tunawashauri Waziri Jafo na mwenzake wa Elimu. Prof. Joyce Ndalichako, kuketi pamoja na wataalamu wa kuona ni namna gani ya kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili ili lisiathiri maendeleo ya taaluma ya watoto wetu katika elimu ya sekondari.

Kwa kuwa serikali imedharimia kwa dhati kutoa elimu bure ya msingi hadi kidato cha nne, tunaamini kuwa ukosefu wa madarasa hautakwamisha tena watoto kuingia kidato cha kwanza kwa wakati mwafaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Masihara kwa taka hizi kwenye magari, tunakaribisha milipuko

**USAFI** wa mazingira unatajwa kuwa muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa afya inazingatiwa na kuzuia uwezekano wa binadamu kukumbwa na athari za taka zinazoweza kuhatarisha afya yake.

Kutokana na hilo, mamlaka husika zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kila mtu anazingatia usafi wa mazingira kwenye eneo lake, linalomzunguka na hata anapokuwa safarini.

Kwa mfano, jijini Dar es Salaam baadhi ya daladala zina vifaa vya kutunza taka, ili kwamba abiria anapohitaji kutumia huduma hiyo, anaipanda akiwa katika usafiri huo ili asichafue mazingira.

Hata hivyo, baadhi ya abiria wamekuwa hawaoni umuhimu wa vifaa hivyo na badala yake wanapomaliza kunywa maji, hutupa chupa chini kana kwamba hawaoni vifaa hivyo ndani ya daladala.

Kwa ujumla ni kwamba, kuna baadhi ya abiria ambao si wastaarabu kwa kutupa chupa za maji au mabaki ya vitu walivyokuwa wakila nje kupitia dirishani. Ni jambo la kawaida linashuhdiwa kila kukicha, huku kondakta naye akiwa kimya tu bila kuhimiza usafi.

Hilo ni moja ya matatizo yanayolikabili Jiji la Dar es Salaam, hasa uchafuzi wa mazingira, na inawezekana ni kutokuwapo kwa usimamizi wenye ufanisi au ni ukosefu wa elimu ya usafi wa mazingira.

Ikumbukwe usafi wa mazingira ni muhimu ili kuhakikisha kuwa afya inazingatiwa na kuzuia uwezekano binadamu kukabiliana na athari za taka, kwa kuwa bila kudhibiti hali hiyo, uchafuzi huo unaweza kuwa mkubwa zaidi.

Watu wenye tabia hiyo wanaweza pia kutupa taka zinazoweza kusababisha matatizo ya kiafya ambayo ni kinyesi cha binadamu na wanyama, taka ngumu, majitaka na nyingine nyingi.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, baadhi ya magonjwa ambayo yamekuwa yakiwakumba Watanzania ya mlipuko kama kipindupindu, ambacho kinaelezwa kuwa chanzo ni kutozingatia usafi wa mazingira.

Mtindo wa kutozingatia usafi wa mazingira, umekuwa ukisababisha baadhi ya watu kutiririsha maji ya vyooni mitaani na hata kuibua harufu kali, ambayo ni hatari kwa afya za watu.

Imekuwa kawaida kukuta taka barabarani, nikitoa mfano wa jijini Dar es Salaam, katika barabara kuu kama ya Morogoro, inayotumika kwa ajili za safari za kuelekea katika mikoa mbalimbali nchini, hata safari za nchi jirani.

Hali inakuwa ya aina hiyo, huku kukiwapo kampeni kutoka kila halmashauri za kupambana na usafi wa mazingira, ikifanywa kwa kuweka kanuni na tozo mbalimbali za kudhibiti mtindo huo. Nasikitika kuna baadhi ya watu hawaoni umuhimu huo.

Katika suala la usafi wa mazingira, uwajibikaji ni muhimu kuhakikisha mabadiliko yanatokea, kwa maana kwamba kila mmoja atambue na kuzingatia usafi wa mazingira kwa ajili ya afya yake.

Elimu ya Afya iendelee kutolewa kila mara, ikiambatana na vifungu vya sheria husika dhidi ya wanaopuuza utekelezaji wa elimu hiyo, ili wachukuliwe hatua zinazostahili kwa ajili ya usalama wa afya zao na wengineo.

Serikali inaweza kuhamasisha ujasiriamali wa taka, huku makondakta nao wakiwa na vituo maalumu vya kuweka taka zinazokusanya ndani ya magari yao ya abiria ili zitumiwe na wajasiriamali.

Ninashauri, kwa sababu hivi sasa kuna vikundi na kampuni nyingi zinazofanya ujasiriamali kutokana na taka, itakuwa vizuri kuhamasisha watu wa vikundi na watu wa mabasi kuzingatia hilo.

Hilo likifanyika litakuwa limetunza mazingira, pia kulinda afya za watu, kuliko ilivyo sasa watu wanatupa taka ovyo na kudai kwamba wapo wanaofanya usafi na kulipwa fedha.

Ninajua kwamba, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaweza kutumika njia mbili, kumlipisha faini yule aliyetupa taka eneo lisilo rasmi au kumzawadia yule anayetoa taarifa juu ya uchafuzi wa mazingira.

Pamoja na njia hizo kutumika, bado ipo haja ya kuendelea kuelimisha umma zaidi kuhusu madhara ya kiafya yanayoweza kusababishwa na uchafuzi wa mazingira, ili hali hiyo isiendelee kujitokeza.

Usafi wa mazingira usifanyiwe kampeni za muda mfupi, bali ziwe za muda mrefu na ziendane na sheria ndogo zitakazowabana wahusika ili hatimaye waogope kutupa taka ovyo.

# Mkuu Wilaya apiga marufuku maegesho magari vichochoroni

**Na Happy Severine,** MASWA

MKUU wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Aswege Kaminyoge, amepiga marufuku uegeshaji wa magari madogo ya abiria katika mitaa mbalimbali mjini badala yaegeshwe kituo kikuu cha mabasi na vituo vidogo vilivyowekwa rasmi kwa ajili ya kazi hiyo.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na mkuu huyo wa wilaya wakati akizungumza na wadau wa usafirishaji katika ukumbi wa ofisi yake mjini hapa.

Alisema halmashauri ya wilaya ilijenga kituo hicho chenye nafasi kubwa kwa ajili ya mabasi na magari yote yanayofanya biashara ya kusafirisha abiria, lakini anashangaa kuona baadhi yanaegeshwa katika vichochoro.

"Tumejenga kituo kikuu cha mabasi mjini Maswa na hiki kinatumika kwa magari yote ya abiria na yale makubwa yaani mabasi na yale magari madogo ambayo mengi yanakwenda maeneo ya vijijini. Wako wanaokuja kuegesha katika kituo hicho, lakini mengine yanaegeshwa kwenye mitaa tena uchochoroni, suala hili halikubaliki," alisema.

Kaminyoge alisema uegeshaji huo usio rasmi umekuwa ukiisababishia hasara halmashauri kwa kukosa ushuru, hivyo kuifanya ishindwe kufikia malengo yake ya kuwahudumia wananchi kupitia mipango ambayo wamejiwekea.

"Suala hili limekuwa kero sasa katika mji wa Maswa. Naagiza wote wanaohusika kulishughulikia na Jeshi la Polisi mhakikishe maegesho yote yasiyo rasmi yanaondolewa. Tumeshuhudia ajali zilizopoteza maisha ya watu kutokana na kuwapo kwa maegesho hayo, hivyo kamateni magari yote na watozeni faini na wakizidi wafikisheni mahakamani," alisema.

Pia aliwataka madereva wa magari hayo kuheshimu sheria na taratibu zinazowataka kuegesha magari katika maeneo yaliyotengwa na halmashauri, ili kuepusha kutolipa mapato ya serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani wilayani Maswa, Samwel Mwanga, alisema sheria ya mipango miji inatoa mwongozo wa kupanga mji na si kufanya shughuli na kukaa holela hata katika maeneo yasiyo rasmi.

Alisema kwa sasa watafanya ukaguzi wa kimya kimya, ili kuwabaini madereva wote wanaokiuka sheria zote za usalama barabarani ambao ndio wamekuwa chanzo cha ajali wachukuliwe hatua za kisheria, wakiwamo hao wanaogesha magari kwenye maegesho yasiyo rasmi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Vivian Christian, alisema msimamo wao ni magari yote yaegeshwe katika maeneo maalumu yaliyotengwa, kinyume cha hapo ni makosa.

# Viwanda 20 vyajengewa uwezo utaalamu

**Na Joseph Mwendapole**



VIWANDA 20 nchini vimenufaika na mradi wa kujenga uwezo wa wataalamu na wafanyakazi wake unaoendeshwa na Shirika la GIZ la Ujerumani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Leodegar Tenga, (pichani) alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku moja wa mrejesho kuhusu mradi huo uitwao 'GIZ Creating Perspective project'.

Alisema mradi huo umesaidia viwanda vingi nchini kujengewa uwezo wa kuongeza uzalishaji na kuboresha bidhaa wanazozalisha ili kushindana na wenzao duniani.

"Ili mtu apate mafanikio lazima ajifunze kutoka kwa mwenzake. Lazima ajue mwenzake anafanya nini ndiyo sababu mradi huu ni muhimu sana kwetu na umekuja kwa wakati mwafaka," alisema.

Tenga alisema kupitia mradi huo, baadhi ya wenye viwanda na wafanyabiashara nchini wametembelea Ujerumani kuangalia namna wenye viwanda huko wanavyozalisha bidhaa na wamefurahishwa na uzoefu walioupata.

Kuhusu shughuli zinazofanywa na CTI kwa msaada wa Shirika hilo la GIZ, Mratibu wa Mafunzo wa Shirikisho hilo, George Selestine, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo ya namna ya kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali viwandani.

Alisema kupitia GIZ walitembelea viwanda 37 kwenye mikoa ya Arusha, Mwanza na Tanga na kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu kodi na ununuzi.

Selestine alisema kupitia msaada wa GIZ, shirikisho hilo limeanzisha Tuzo za Rais za Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA). Alisema viwanda vinavyofanya vizuri zaidi vimekuwa zikipewa tuzo mbalimbali kama motisha wa kuendelea kufanya vizuri.

Alisema kupitia msaada wa GIZ wanatarajia kuendelea kusaidia wanachama wa Shirikisho hilo kuboresha shughuli zao na kutoa mafunzo ya aina mbalimbali ambayo yatakuwa msaada kwao.

Lydia Koch ambaye ni mshauri wa GIZ Creating Perspective, alisema mradi huo ni jitihada za pamoja kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Shirikisho la Wenye Viwanda Ujerumani, Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) na GIZ.

Alisema mradi huo umevitambua viwanda 74 kwa ukanda wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kuvipa mafunzo ya kitaalamu ili viboreshe uzalishaji wa bidhaa zao.

Koch alisema viwanda hivyo vimenufaika kwa kupata mafunzo, huduma za ushauri kutoka kwa wataalamu wa Ujerumani na kuanzisha uhusiano imara baina ya viwanda vya Afrika Mashariki na vila vya nchini Ujerumani.



# Shein ataka mahafali OUT Zanzibar

**Na Vincent Mpepo,** OUT

RAIS mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (pichani), ameushauri uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) uhakikishe mahafali ya chuo hicho yanafanyika visiwani Zanzibar kwa kuwa yote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Shein alitoa rai hiyo jana, wakati wa mahafali ya 39 ya chuo hicho yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Bungo, Kibaha mkoani Pwani. Alisema anatambua utaratibu wa chuo hicho kufanya mahafali katika vituo vyake vya mikoa, hivyo kushauri ikiwezekana kwa wakati ujao mahafali yafanyike Zanzibar.

Vilevile, Mkuu huyo mpya wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, aliwataka wahitimu kutumia elimu waliyoipata kubuni na kupata majibu ya matatizo yanayoikabili jamii.

"Mliohitimu mnapaswa kuwa mabalozi wazuri wa kuitekeleza kwa vitendo dhana ya uzalendo na uwajibikaji unaotanguliza mbele maslahi ya umma," alisema.

Makamu Mkuu wa OUT, Profesa Elifas Bisanda, alibainisha kuwa waliohitimu katika chuo hicho mwaka huu ni 2,996 na kati yao, wanawake ni 1,282.

Akitoa neno la shukrani kwa mgeni rasmi, kiongozi huyo wa chuo aliwataka wahitimu kujiuliza baada ya kutunukiwa vyeti, astashahada na shahada mbalimbali wataifanyia nini jamii na chuo.

Alisema hadi kufikia mahafali ya 38, jumla ya wahitimu 43,562 wametunukiwa vyeti, astashahada na shahada mbalimbali kufanya idadi kufikia wahitimu 46,558 kwa sasa.

Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Profesa Rwekaza Mukandala, alisema pamoja na chuo hicho kutoa elimu kwa njia ya huria na masafa, bado kuna kikwazo cha kutoeleweka kwa chuo hicho kwa jamii na hata baadhi ya wasimamizi, kitu ambacho kinakilazimu kujitangaza kupitia vyombo vya habari.

Mwenyekiti huyo alisema baraza lake limefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kusimamia vyema matumizi ya rasilimali watu na fedha, hivyo kupata hati safi ya ukaguzi.





Baadhi ya wajumbe wa kamati ya kitaifa ya kusukuma mashauri ya madai, ambao ni majaji wafawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, wakifuatilia kikao cha uzinduzi wa kamati hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Halmashauri yapoteza mil. 10/- kila mwezi

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

HALMASHAURI ya Songea, mkoani Ruvuma inapoteza mapato ya Sh. milioni 10 kila mwezi kutokana na kituo cha mabasi Kata ya Sheluyatanga kutotumika.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameliagiza Baraza la Madiwani la Manispaa ya Songea ifikapo Desemba 31, mwaka huu, kituo hicho kianze kufanyakazi.

Alitoa agizo jana wakati akizungumza kwenye Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, muda mfupi baada ya madiwani hao kula kiapo cha kuwatumikia wananchi.

Mndeme alisema kutokufanya kazi kwa kituo hicho kunapoteza mapato mengi ndani ya halmashauri takribani Sh. milioni 10 kwa mwezi kupitia miundombinu iliyowekwa ikiwamo vyumba 30 ambavyo pango lake siyo chini ya Sh. 80,000 kwa mwezi. Alisema kuwa hayupo tayari kuona fedha zilizotafutwa na Rais Dk. John Magufuli zilizojenga kituo hicho zaidi ya Shilingi bilioni sita zinapotea kwa uzembe, jambo ambalo halikubaliki.

Alifafanua kuwa ili kufanikisha kituo hicho kinafanyakazi, daladala zote ni lazima zifike katika kituo hicho mapema pamoja na kukifunga au kukifuta kituo cha mabasi cha Kata ya Msamala kwa lengo la kukipatia nguvu kituo cha Shuleyatanga. Pia, alilitaka baraza hilo kusimamia machinjio Kata ya Shuleyatanga yaanze kufanya kazi ili mapato yaingie ndani ya halmashauri hiyo. Kwa upande wake, Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano, wakati akipokea agizo hilo kwa niaba ya madiwani wote alisema kuwa baraza hilo lipo tayari kuyafanyia kazi yote yaliyoagizwa.

## Diwani aahidi neema Tabata

**Na Maulid Mmbaga**

DIWANI mteule wa Kata ya Tabata kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Omary Matulaga, amewashukuru wanachama na wananchi wa kata hiyo kwa kumwezesha kushinda katika kinyang'anyiro hicho na amewaahidi kutowaangusha.

Akizungumza na wananchi wa kata hiyo jana, alisema kwa kushirikiana na Serikali Kuu atahakikisha anatatua changamoto za wananchi zilizokuwa zikipigiwa kelele kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita katika kata hiyo ikiwa chini ya uongozi wa upinzani.

Alisema baada ya jitihada na kazi kubwa waliyoifanya imewafanikisha kurudisha kata hiyo, chini ya CCM na ni wajibu wake kuhakikisha anayatimiza aliyowaahidi wananchi kwa kushirikiana na Serikali Kuu.

"Sisi na Rais John Magufuli kila tulipopita na kuziona shida na changamoto za wananchi tuliahidi tutaisimamia ilani ya CCM na tutazitatua changamoto hizo na harakati za kutafuta maendeleo katika kata yetu zitaendelea," alisema Matulanga.

Aliongeza kuwa katika kata hiyo miaka mitano iliyopita ikiwa chini ya uongozi wa upinzani, walikuwa wakiomba kuboreshewa miundombinu, gari la taka na mikopo kwa kinamama na vijana na hakuna kilichofanyika.

Alisema katika uongozi wake atahakikisha hayo yote yanatekelezwa kwa wakati pia aliwataka viongozi wa kata, matawi na mashina kutumia nafasi zao kusimamia na kutekeleza ilani ya chama hicho.

"Niwaombe viongozi wa CCM kutumia nafasi zenu kutuongoza, kutushauri na kutusimamia katika utekelezaji wa ilani ya chama chetu, pia tutumie muda wa vikao vyetu vya chama kutafuta shida na changamoto za wananchi na kuzitatua," alisema Matulanga.

Aliwashauri viongozi wengine wa chama hicho kushirikiana katika majukumu yao badala ya kutumia muda mwingi kulaumiana kwa kuwa kwa kufanya hivyo hawataweza kufikia malengo waliyowaahidi wananchi.

HABARI KITAIFA

# Jela miaka 10, kulipa faini ya 200,000/- kwa kubaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa Wete, imemhukumu kifungo cha miaka 10 jela na kulipa fidia ya shilingi 200,000 mshitakiwa Khalifa Khalfan Mwaveso (25), mkazi wa Micheweni Pemba kwa kosa la kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 17.

Baada ya mahakama kufanya uchambuzi wa Sheria juu ya ushahidi uliwasilishwa na upande wa mashtaka, mahakama imethibitisha kosa pasi na chembe ya shaka.

Baada ya hapo Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, alitoa hukumu hiyo chini ya kifungu cha 210 cha Sheria namba 7 ya mwaka 2018.

Pia alimwamuru mshtakiwa kulipa fidia ya shilingi 200,000 kama fidia kwa muathirika ndani ya siku 14.

Kabla ya hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Pemba, Juma Mussa Omar, alidai hawana kumbu kumbu za awali za mshtakiwa huyo, ingawa aliiomba mahakama kutoa adhabu kali, ili iwe fundisho kwa wengine.

Kwa upande wake mshitakiwa huyo aliiomba mahakama impunguzie adhabu angalau, impatie adhabu ya kwenda kuitumikia jamii.

Awali ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa siku na tarehe isiyojukana Oktoba mwaka 2019 saa 3:00 usiku huko Pandani Masipa Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali, alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 17.

Kufanya hivyo ni kosa kinyume na kifungu cha 108 (1) (2) (e) na kifungu cha 109 (1) vya Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

Kesi hiyo namba RM 04/2020 ilianza kusikilizwa katika Mahakama ya Mkoa Wete Januari 1, mwaka huu.



Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, akimpa maelezo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Jenista Mhagama, alipokuwa akikagua maendeleo ya ukarabati wa kumbi za Bunge pamoja na Ofisi za Bunge. **PICHA: BUNGE**

# Mabula aziweka kikaangoni kampuni urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kampuni zote zilizochukua fedha za wananchi kwa ajili ya urasimishaji na kushindwa kufanya kazi hiyo, kupelekwa kwenye vyombo vya sheria.

Dk. Mabula alitoa maagizo hayo jana jijini Mwanza, alipofanya ziara ya kushtukiza katika ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Mwanza kukagua utendaji kazi wa kampuni binafsi zinazoendesha urasimishaji na kufuatilia ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na utoaji hatimiliki kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kutoridhishwa na urasimishaji makazi, kazi iliyokasimishwa kwa kampuni binafsi za upimaji.

Alisema kampuni hizo zimechukua fedha za wananchi, huku kasi ya umilikishaji ikiwa ndogo kulinganisha na mwitikio wa wananchi.

Pia alisema wananchi wamekuwa wakilalamikia utoaji hati kwenye ofisi za ardhi kuchukua muda mrefu tofauti na ilivyoelekezwa. Kutokana na hali hiyo, alitoa mwezi mmoja kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Biswalo Makwasa, kuhakikisha anashughulikia kero hiyo.

Kuhusu makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, Dk. Mabula alionyesha kutoridhishwa na kazi hiyo, huku akibainisha kuwa malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni Sh. bilioni 200, lakini hadi Novemba, mwaka huu, Sh. bilioni 50 zilikusanywa jambo alilolieleza kuwa bado zinahitajika juhudi kubwa ili kufikia malengo.

Kwa upande wake, Makwasa alisema mbali na kuahidi kutekeleza maagizo ya Naibu Waziri, ziara hiyo ni chachu ya ofisi yake kuongeza kasi katika utendaji kazi ili kufikia malengo.

Kwa mujibu wa Biswalo, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Mwanza sasa inaendelea na utoaji ankara za umilikishaji kwenye maeneo yaliyorasimishwa katika halmashauri za Mkoa wa Mwanza sambamba na kupeleka timu ya wataalamu wa ardhi kwenye halmashauri za wilaya za Buchosa, Sengerema, Ukerewe na Magu kwa ajili ya kutoa elimu na kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi.

Naye Msajili wa Hati Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Ivan Amurike, alisema moja ya changamoto zinazochangia ofisi ya ardhi kupunguza kasi ya utoaji hati na ukusanyaji kodi ya pango la ardhi ni kutojitokeza kwa wamiliki wa ardhi kuchukua hati miliki pindi zinapokamilika.

## Ndikilo ataka maboresho ya barabara za mjini

**Na Futuna Selemani,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, ameagiza kuboreshwa kwa barabara zilizopo maeneo ya mjini kwa kuwa eneo hilo limekaa vibaya.

Baadhi ya barabara hizo ni ya mzunguko kwenye eneo la Nida kuelekea soko la Loliondo na stendi mpya ya Maili Moja mjini Kibaha.

Ndikilo alitoa maelekezo hayo katika ziara ya kukagua baadhi ya miradi ya barabara kwenye wilaya za Kibaha na Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo.

Ili kazi hiyo ifanyike, aliutaka Wakala wa Barabara (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoa wa Pwani kuhakikisha wanasimamia miradi muhimu ya barabara iliyopo kwenye mkoa huo, ili ikamilike kwa wakati.

"Kabla hamjapata fedha kiasi cha Sh. milioni zaidi ya 400 rekebisheni kwanza kwa kiwango cha changarawe," alisema Ndikilo.

Alisema miradi hiyo ni muhimu kwani itasaidia kuleta maendeleo ya wananchi kwa kurahisisha usafiri na katika kuinua uchumi wa mkoa pamoja na vipato vya wananchi kwenye maeneo yenye miradi hiyo.

Mratibu wa TARURA mkoa wa Pwani, Lutufyo Mwakigonja, alisema utekelezaji wa miradi iliyo chini yao inatekelezwa kulingana na bajeti.

Alisema katika kuhakikisha miradi ya ujenzi wa barabara inakuwa na mafanikio, wanashirikiana na wananchi kwenye maeneo ya miradi ikiwamo kuwapa elimu juu ya umuhimu wa miradi hiyo.

Meneja wa Tanroads Mkoa wa Pwani, Yudas Msangi, alisema miradi inayoendelea iko kwenye hatua nzuri.

Msangi alisema watahakikisha inakamilika kwa wakati, ili iwaondolee adha wananchi na kuwaletea maendeleo, kwani ni moja ya nyenzo za maendeleo.

# Waziri NEMC kuziimarisha ofisi za kanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Ummy Mwalimu, amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kuimarisha ofisi zake za kanda na kuwajengea uwezo wafanyakazi ili wamudu kasi ya uwekezaji nchini.

Akizungumza na Menejimenti ya NEMC jijini Dar es Salaam, Waziri Ummy alisema NEMC haipaswi kuwa kikwazo kwa namna yoyote ile kwa wawekezaji.

Tunahitaji kufanyakazi kwa kasi kubwa ili kukidhi mahitaji ya wawekezaji na hilo litawezekana kama NEMC mtaimarisha ofisi za kanda kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi waliopo kwenye ofisi hizo ili kuondoa mrundikano wa mambo hapa makao makuu ya baraza, amesema.

Amesema uchumi wa viwanda utafikiwa kwa kuwekwa mazingira mazuri ambayo wawekezaji watavutika na kuja kuwekeza na hilo linawezekana kama taasisi zote zitajipanga kwa kuweka mikakati mizuri.

NEMC mbali ya kusimamia mazingira lazima pia mhakikishe mnasimamia miradi ya kimkakati ambayo inatekelezwa na serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, alisema na kuongeza kuwa NEMC haipaswi kuwa kikwazo katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Aidha, Waziri Mwalimu amesema baraza lifanye pia kazi ya kuwashuri wawekezaji licha ya uwepo wa wataalamu elekezi kwani baadhi yao siyo waaminifu amesama na kufafanua kwamba hao wachache wamekuwa wakirefusha michakato ya upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji ikiwamo utoaji wa vibali.

Tusibaki tu ofisini huku tukiamini kuna wataalamu elekezi ambao wachache kwa maslahi yao wamekuwa wakichelewesha mchakato wa baadhi ya huduma na hivyo kuipa doa NEMC. Mnayo nafasi ya kushauri wawekezaji ili waweze kupata wataalamu elekezi ambao wapo makini na kazi zao jambo ambalo litaondoa malalamiko yasiyo na ulazima kwenu, alisema.

Waziri Ummy aliwakumbusha Watanzania umuhimu wa kutunza mazingira kwa faida ya kizazi cha leo na cha baadaye.

Siku za karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la joto dunia na ii inatokana na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za binadamu.Nawakumbusha Watanzania kuyatunza mazingira ili nayo yatutunze,

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema watayafanyia kazi mapendekezo yote ya Waziri yanayohusu menejimenti na watumishi.

Baraza limejipanga kutekeleza na kusimamia miradi yote ya kimkakati kwa ufanisi mkubwa na baada ya maelekezo ya waziri itakuwa rahisi kutekeleza mipango yetu kwani mingi ya mikakati aliyoelekeza tulikwishanza kuitekeleza na hata mikakati ambayo bado hatujaanza utekelezaji wake tutaitekeleza kwa maelezo aliyotupa Waziri," alisema Dk. Gwamaka.

NEMC ina ofisi za kanda sita katika Kanda ya Kati (Dodoma), Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Kusini (Mtwara) na Kaskazini (Arusha).




Meneja Mwandamizi wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Abel Lasway (katikati), akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari wakati wa kutangaza washindi wa kampeni ya JIPE 5 na Scholar ambayo inaendeshwa na Benki ya CRDB kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo hapa nchini. Kulia ni Meneja wa Udhamini na Matukio wa benki hiyo, Lilian Kanora na Evance Mkao ambaye ni Meneja Uhusiano Upande wa Mauzo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasiokuwa na vyoo waanza kukaguliwa Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KAMATI ya Mazingira Mtaa wa Tangini, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, imeanza kukagua wananchi wasiokuwa na vyoo bora pamoja na kudhibiti utupaji taka ovyo kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Shauri Yombayomba, alisema hayo wakati akiongea na waandishi wa habari.

Alisema kamati hiyo imeanza kazi yake mwezi Novemba kwa kutembea nyumba hadi nyumba na kukagua hali ya vyoo na namna ya utunzaji wa mazingira.

Alisema kamati hiyo ilibaini uwapo wa tundu moja la choo kwenye nyumba yenye wapangaji zaidi ya familia 10 hali ambayo ni ya hatari, pia utiririshaji wa maji machafu kwenye eneo ambalo si salama kwa wananchi.

"Kamati hii pia imebaini baadhi ya kaya kutokuwa na vyoo, na pia wapo wafugaji wadogo wanatiririsha maji kwenye makazi ya watu hali ambayo ni ya hatari inayoweza kusababisha mlipuko wa magonjwa," alisema Shauri.

Alisema, wananchi waliobainika kuwa katika hatari ya kusababisha magonjwa ya mlipuko katika mtaa huo wameitwa na kuonywa na kuingia mkataba wa kurekebisha kasoro zao.

Alisema baadhi yao ambao walikaidi wito wa barua wataitwa tena na wasipotokea hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ili kuweka mazingira safi katika mtaa huo.

Shauri alisema kamati hiyo inaendelea kuzunguka katika mtaa huo nyumba hadi nyumba na kukagua maeneo ya kuhifadhia taka.

# Watoto wa kike walia na wazazi kuendeleza unyanyasaji kijinsia

**Na Christina Haule,** MVUHA

SERIKALI imeombwa kutoa elimu kila mara kwa wazazi juu ya umuhimu wa shule kwa watoto wa jinsi zote, ili waache tabia ya kufanya ubaguzi kielimu kwa kumwona mtoto wa kiume ni bora kuliko mtoto wa kike.

Habiba Shabani (12), mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Mvuha, alitoa ombi hilo kwenye kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto zilizofanyika katika kata ya Mvuha wilayani Morogoro.

Shabani alisema kitendo cha watoto wa kike kubaguliwa kinaendelea katika wilaya hiyo, huku akidai kuwa mtoto wa kike anaonekana anastahili kubaki nyumbani na kusubiri kuolewa huku mtoto wa kiume akionekana ana umuhimu wa kupelekwa shuleni.

"Kubaguliwa mtoto wa kike kwa kuambiwa abaki nyumbani na mtoto wa kiume kupewa kipaumbele kwenda shule kusoma ni ubaguzi ambao ni sehemu kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia. Haifai na sisi tunataka kwenda shule, wazazi wanapaswa kuelimishwa," alisema.

Naye Meneja wa Taasisi ya Kuhudumia Wakimbizi ya Tanganyika (TCRS), Rehema Samuel, aliwapongeza waanzilishi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kutokana na matamasha hayo kuonekana kuelimisha jamii maana ya ukatili wa kijinsia na nini wafanye kuepukana na ukatili huo.

Alisema katika Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, walibaini uwapo wa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii kuwa ni vingi ikiwamo watoto wa kike kukeketwa kitendo ambacho kinapigwa marufuku kila siku.

Samuel alisema pia walibaini kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji unaofanywa na ndugu na jamaa wa karibu na mtoto na kwamba na vinasababisha familia kushindwa kuishi kindugu kwa kutoelewana.

Akizungumzia kaulimbiu ya mwaka huu, 'Tupinge Ukatili wa Kijinsia, Mabadiliko Yanaanza na Mimi', Samuel alisema imehimiza wanaume, wanawake na watoto kujitokeza katika kupata elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali inayojihusisha na utoaji elimu ya sheria mbalimbali ikiwamo kupinga ukatili (Morogoro Rural Paralligal Center- Matombo), Asha Kungubaya, alisema wanawake 250 wameshapatiwa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kutokana na wanawake wengi, hasa wa vijijini, kuwa wagumu kuelewa maana ya ukatili wa kijinsia.

Alisema akiwa kiongozi mwanamke, ameona changamoto kubwa ni wanawake wengi bado wagumu kuelewa elimu ya ukatili wa kijinsia na anapaswa kutengewa muda wa kutosha na kuelimishwa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Morogoro, Florence Mwambene, akisoma risala ya wilaya ya siku hiyo, alisema kamati 22 za MTAKUWWA kati ya 31 zimeundwa tangu kuzinduliwa kwa maadhimisho ya siku 16 wilayani humo, ili kusimamia masuala ya kijinsia.

Pia alisema tayari kesi 64 za ukatili wa kijinsia kwa watoto na 96 za wanawake zimeshashughulikiwa ikiwa ni mchanganyiko wa matukio ya kubakwa, vipigo na kutelekezwa.

Mwambene alisema kupitia Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wanawake 60 waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali, walijengewa uwezo wa kujiamini na kupambana na changamoto zinazowakumba wanawake wakati wa mchakato mzima ikiwamo rushwa ya ngono.



Ukurasa 12

Kahama yaja na staili pembejeo bure kwa vijana kukuza kilimo na ajira zao


# BUFE

IJUMAA DESEMBA 18, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

Tarime yawekeza uchumi katika majengo yatakayoingiza mamilioni kodi, ajira kibao

# Umaskini unavyopigwa deki Kibaha kupitia msaada sheria

- Kinara watoto wanaotelekezwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA



Mkuu Kituo Cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), Catherine Mlenga, katika moja ya mikutano yake. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

BAADHI ya wanawake wanaonyanyasika na wanaume waliofunga nao au wamezaa na watoto bila ya ndoa, hawaishi pamoja hata wakihanagika.

Baadhi ya wazazi wamekuwa kikwazo kwa watoto kuwa na maendeleo bora masomoni, kutokana na wazazi kuhama wakitafuta kazi za kuwawezesha kulea familia.

Baada ya kubaini adha hizo, kumeanzishwa Kituo Cha Msaada wa Kisheria Kibaha (KPC), ambacho sasa kinaonyesha ukombozi kwa wanawake kupitia elimu ya sheria. Mkurugenzi wa KPC, Catherine Mlenga, anaelezea walivyowanusuru kinamama wanaonyanyasika kwenye familia zao na hawakujua pa kupata msaada.

Mkurugenzi huyo anaeleza, KPC ilianzishwa zaidi ya miaka 10 iliyopita na imekuwa ikitoa msaada wa sheria bure kwa kinamama, wanaume na watoto.

Anasema elimu katika kata 14 za Halmashauri ya Mji wa Kibaha, tayari imetolewa na wataendelea katika maeneo mbalimbali, ikihusu sheria ya mtoto, ndoa, mirathi, ukatili wa kijinsia na umiliki wa ardhi.

"Tumefanikiwa kuwafikia viongozi wa kata, vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA) na wananchi katika maeneo mbalimbali ya mji wa Kibaha" anasema.

Anarejea takwimu kuwa mwaka 2017, walipokea wahitaji wa msaada wa kisheria 583, wanawake 327 na wanaume 256, sehemu kubwa ya malalamiko ni matunzo ya watoto, wakifuatiwa na kesi za ndoa na mirathi.

Hata hivyo, anasema takwimu za mwaka jana zinaonyesha wamepungua hafi kufikia 140 na Catherine anajivuna kuwa kasi ya elimu waliyoitoa sasa inaonyesha mafanikio, kwa wengi kutambua haki zao.

Anasema kesi za ndoa na ukatili wa kijinsia wamezifuatilia na kubaini zinachangiwa na wanaume kuchepuka, huku wakisahau kuhudumia familia zao.

Sababu ni kipato kidogo cha wanaume, kinachowakwamisha kumudu kuhudumia familia na wanaangukia kuitelekeza familia, kwenda kusikojulikana.

" Kwa upande wa wanawake ndoa zao zinavunjika kwa kutafuta wanaume wenye ahueni ya kipato, jambo linalosababisha kuendelea kuzaa watoto kila mmoja na baba yake," anasema, huku akidokeza wazazi kutengana, pia chanzo cha ukatili kwa watoto kukosa haki za msingi kama elimu.

Kuhusu ukatili wa kijinsia, mkurugenzi huyo anasema vipigo kwa wanawake ni hali inayopaswa kukemewa kwenye jamii na kuwaelimisha wawe na sauti katika utafutaji haki zao kisheria.

"Pamoja na kutoa elimu katika ofisi yetu iliyopo Kibaha Mjini, tunaendelea kutoa msaada wa kisheria bure kwa watu wote.

"Mlalamikiwa anayetajwa, tunatoa barua ya kumuita na kuwashauri kwa pamoja, ikishindikana tunaandika barua nyingine afikishwe ustawi wa jamii kwa hatua zaidi" anaeleza Mkurugenzi Catherine.

Anaendelea kuwahamasisha wananchi kufika kupata msaada wa kisheria katika kituo hicho, ili kila mmoja ajue haki yake na pindi anapobaini imekiukwa aende sehemu inayostahili.

Mkurugenzi huyo anasema, kujiamini ni moja ya silaha anayoitumia kufanikisha uongozi wake, kato ya vituo tisa violivyokom mkoa wa Pwano.

Anaiomba serikali kufikisha Elimu ya ya ukatili wa kijinsia kuanzia shuleni, ili kukomesha hali hiyo kwa jamii, sambamba na wizara husika kuwezesha vituo vya msaada wa kisheria, ili wahitaji ambao ni wa kipato cha chini wamudu kunufaika.

Mmoja wa wanufaika aliyejitambulisha kwa jina moja la Mayasa, anakiri KPC Kibaha imemsaidia kupata haki yake na anampongeza Mkurugenzi kuwasaidia wahitaji.

Mratibu wa vituo vya msaada wa kisheria vilivyopo mkoani Pwani, Francis Johnson, anatumia nafasi kuwasisitiza wanawake kuwa viongozi bora kwenye maeneo wanayoaminiwa na kupewa nafasi.

BIASHARA

# Kahama yaja na staili pembejeo bure kwa vijana kukuza kilimo na ajira zao

• Bwana Shamba bure, sharti kulima ekari 5 • Wazembe wajitoa walipogundua 'hamna keshi'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama, imo katika orodha cha zinazotenga fedha kila mwaka kupitia mapato yake kwa ajili ya kununua ruzuku za pembejeo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35.

Vijana hao ni wenye uwezo wa kulima mazao ya biashara na chakula kuanzia ekari tano na kuendelea na mazao wanayoyapata yanabaki kuwa mali zao.

Ni mradi unaonasimamiwa na maofisa ugani wake wa kila kata, kuhakikisha wanalima kitaalamu na kuzalisha mazao kwa wingi.

Lengo la utoaji ruzuku za pembejeo za kilimo kwa vijana, ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya kibiashara hasa mpunga, mahindi, alizeti, pamba na mtama, sambamba na kutatua changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana hao waliohitimu masomo wanaobaki mitaani bila shughuli maalum.

Halmashauri hiyo ina wajibu kulisha na kuzalisha malighafi ya viwanda, kutoka mazao ya kibiashara ambayo yamekuwa msaada kwa uendeshaji viwanda hivyo.

Hadi sasa ni kipindi cha miaka mitatu sasa halmashauri ina utaratibu wa kutenga fedha kupitia mapato yake ya ndani na kugharamia ruzuku za kilimo, zinazowasaidia wananchi kuinuka kiuchumi, kwa kuwa wakulima wenye uwezo wa kuzalisha mazao msaada wa malighafi kwa viwanda nchini.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba (aliyevaa miwani), akizungumza na wakulima vijana 45 waliolima mashamba ekari tano na kuendelea za mazao ya chakula na biashara, baada ya kuwakabidhi ruzuku za pembejeo bure zinatolewa kila mwaka. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

### DED KAHAMA MJINI

Anderson Msumba, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema ni miaka mitatu mfululizo wamekuwa wakitenga fedha kupitia mapato yake ya ndani, kununua pembejeo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye umri miaka 18 hadi 35.

Anaziainisha ruzuku hizo ni pembejeo zinazotolewa bure ni mbolea za kupanda (NPK), mbegu za mahindi na alizeti, sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba na mavuno yanayopatikana ni mali yao.

Katika mwaka uliopo wa fedha, Halmashauri imetenga Sh. milioni 72 za kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa vijana wanaolima mazao ya chakula na biashara, lakini walijitokeza wachache na kusababisha fedha kurudi kila msimu.

"Katika halmashauri zote nchini, halmashauri pekee inayotoa ruzuku za kilimo bure kwa vijana ni halmashauri yetu, mvua zimeanza kunyesha na vijana mnatakiwa kuchangamkia fursa hii kwa ajili ya kilimo chenye tija hasa kwenye mazao ya chakula na biashara.

> **Ni vyema vijana wakajitokeza kujiandikisha kwenye ofisi za serikali za vijiji na kata kwa ajili ya kupata pembejeo msimu ujao.**



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, akimkabidhi mkulima kijana, Lazaro Kafumo kutoka Kata ya Mwendakulima, mbolea ya kupanda na kukuzia mazao.

"Msimu huu tumetoa pembejeo kwa zaidi ya vijana 545, watalima ekari 725 ya mazao ya chakula na biashara. Hivyo, msimu ujao tutawagawia vijana wengine mbali na hawa tuliowapatia pembejeo.

"Ni vyema vijana wakajitokeza kujiandikisha kwenye ofisi za serikali za vijiji na kata kwa ajili ya kupata pembejeo msimu ujao," anasema Msumba.

Anasema, mtu anapokaguliwa eneo lake la kilimo na maofisa ugani wa kata wanamshauri aina ya mazao ya ya kulima na kisha wanafanya ziara za kuwakagua na kuwapa ushauri wa kitaalamu.

### OFISA KILIMO

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama Samson Sumuni, anasema walianza kutenga bajeti ya kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana, tangu mwaka wa fedha 2018/2019.

Anasema mgawanyo wake, Sh. milioni 54 na mweka huo walinunua mbolea za kupandia (NPK) kilo 139; mbegu za mahindi kilo 360; mbegu za alizeti kilo 75 ambazo walipatiwa wakulima vijana 27, waliolima mashamba jumla ya ekari 139.

Sumuni anasema, katika mwaka wa fedha uliofuata wa 2019/2020, halmashauri Sh. ilitumia milioni 17.7 kununua mbolea za kupandia (NPK) kilo 195; mahindi kilo 550' alizeti kilo 90 na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba chupa 90 na walizigawa kwa wakulima 39 waliolima jumla ya ekari 195.

Katika mwaka uliopo wa fedha, Halmashauri ya Kahama imetenga Sh. milioni 72 na kununua ruzuku za pembejeo za Sh. milioni 24, ambazo ni mbegu za mahindi kilo 785; alizeti kilo 45; dawa za pamba chupa 20; mbolea za kukuza na kupanda mifuko 225 na mbegu za mtama kilo 1,500.

Sumuni anasema, mbegu za mtama zitaelekezwa kwenye kata 15 zinazolima mazao yanayostahimili ukame kulingana na malekezo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, inayobashiri upungufu wa mvua katika Kanda ya Ziwa na ekari 725 za mazao ya chakula na biashara zitalimwa na vijana 45.

"Kuna vijana wengi wako mitaani hawana shughuli ya kufanya na kwa kuliona hili, tulianzisha mpango wa kutoa pembejeo za kilimo bure kwa vijana wenye miaka 18 hadi 35 na wenye uwezo wa kulima kuanzia ekari tano na kuendelea na kila mwaka wanazidi kuongeza," anasema Sumuni.

Anafafanua kuwa, mbali na kuwagawia pembejeo hizo za bure za kilimo, pia wamekuwa wakiwapatia elimu ya namna ya kulima kisasa na kuhifadhi chakula katika mazingira bora, ili mazao yasije kutengeneza sumbukuvu na kuwapatia mbinu kutafuta masoko.

### CHANGAMOTO ZAO

Mkurugenzi Msumba, anasema vijana wengi wanashindwa kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo kutokana na wengi wao hawahitaji fedha kwenda kununua pembejeo, badala yake wanazielekeza kwenye michezo ya kubeti.

Anasema, katika msimu uliopita Halmashauri ilitenga Sh. milioni 50 za kununua pembejeo hizo, lakini walijitokeza vijana wachache ukilinganishwa na idadi ya waliopo wilayani hapo na kusababisha kutumia Sh. milioni 17 pekee, nyingine zikirejeshwa.

"Sisi tunatenga fedha za kununua pembejeo kila mwaka kwa ajili ya vijana mbali na mikopo ambayo hutolewa pia kwa vijana, lakini wanajitokeza wachache na kusababisha fedha kurudi kila mwaka. Wengi wenu mnahitaji 'keshi' jambo ambalo sisi halmashauri sio utaratibu wetu," anasema Msumba.

Sumuni anasema wakulima hawana elimu ya uhifadhi wa mazao ambayo wamekuwa wakiyapata shambani wakati wa mavuno na kwamba wanaendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazao kama mahindi, maharage na pamba, ili zisiharibike na kutengeneza sumbukuvu.

### VIJANA WALIOJITOKEZA

Elizabeth James, mkulima kutoka Kata ya Kinaga katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema awali hakuamini serikali ingeweza kutoa pembejeo bure, hadi msimu uliopita aliposhuhudia wenzake ndani ya kata waliopewa pembejeo na kuvuna mazao zaidi.

Anasema, naye msimu huu amehamasika na kujitokeza kuchangamkia fursa na kabla ya kujitokeza kuchukua pembejeo, alikuwa akitumia samadi kwenye kilimo na kumfanya aambulie mavuno kidogo waliyotumia kwenye chakula cha familia.

Mdadi Emmanuel kutoka Kata ya Kagongwa, anasema uwepo wa pembejeo hizo utasaidia kuongeza uzalishaji mazao ya chakula na biashara kwa wingi, ikilinganishwa na kipindi cha nyuma na anaiomba halmashauri kuwatafutia masoko ya mazao watakayoyapata, ili kujiongezea kipato.

Pia, anatumia fursa hiyo kuipongeza halmashauri kwa kuwapatia pembejeo za kilimo bure, sambamba na maofisa ugani kwa kila kata wanaowatembelea kila mara na kuwapa ushauri wa kitaalamu, kwa lengo la kufanikisha mavuno zaidi.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tuthamini michango ya watu wetu






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

HIVI karibuni baadhi ya Watanzania wakielekeza mawazo yao jijini Berlin, Ujerumani, waliposikia ndugu yao kapewa jina la mtaa katika Jiji hilo maarufu barani Ulaya na duniani.

Mmoja wa waliokuwa mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Tanzania, chini ya Rais Mwalimu Julius Nyerere, alipewa jina la mtaa jijini humo na kuamsha akili za Watanzania kujiuliza imewezekanaje?

Lucy Lameck, ndiye Mtanzania aliyepewa mtaa huo ambao awali ulijulikana kama Von Wissman Strabe na sasa ni Lucy Lameck Strabe. Strabe ni mtaa kwa lugha ya Kijerumani, kama ilivyo street kwa Kiingereza.

Hiyo si heshima tu kwa familia ya Lucy au ukoo wake, achilia mbali kabila lake la Kichagga, bali ni kwa Taifa la Tanzania kwa jumla, kwamba Taifa kubwa kama Ujerumani limetambua kuwahi kuwapo kwa mtu huyo, ambaye sasa anaweka alama ya kudumu Ujerumani.

Pamoja na Watanzania wanaoelewa nini kimefanyika, kujivunia hatua hiyo, lakini ni changamoto kwao na hivyo kulazimika kujiuliza ni wapi wanakwama, hata kushindwa kutambua mchango wa watu wake, mpaka kufunuliwa macho na mataifa mengine.

Tujiulize, hivi Lucy asingetambuliwa na Wajerumani mpaka kupewa kumbukumbu ya mtaa, sisi Tanzania tungemfanyia nini katika kutambua mchango wake kama waziri wa Tanzania chini ya Rais Nyerere?

Tunao Watanzania wangapi wa kaliba ya Lucy waliostahili kupewa kumbukumbu kama hiyo? Je, tumeshajiuliza ni kwa nini mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere hana kumbukumbu ya maana nchini?

Hatujui au hatuoni mchango wake mpaka siku moja tusikie mataifa ya Kusini mwa Afrika, ambako Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alichangia katika kuyapatia uhuru wao, wamempa mtaa, shule, jengo au uwanja, ndipo nasi tuamke?

Nilipata kuhoji huko nyuma, kwamba ni kwanini hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara iliyojengwa Kwangwa mjini Musoma, iliyoanza kujengwa enzi za Nyerere, isingepewa jina la Mama Maria? Sikujibiwa, lakini baadaye nikasikia imepewa jina la Hospitali ya Rufani ya Mwalimu Julius Nyerere!

Pengine kwa kuwa sikuwa na ushawishi, niliishia kugugumia na kuacha liende. Lakini, bado naamini mama huyo anastahili kupewa kumbukumbu kubwa, tena kuzidi hata strabe aliyopewa Lucy jijini Berlin. Ana mchango mkubwa na heshima kama mke wa Rais wa Kwanza wa Tanzania.

Si huyo tu, kuna Watanzania waliofanya makubwa ndani na nje ya nchi na wengine wameshaondoka duniani, lakini hakuna kilichobaki kama kumbukizi zao kitaifa. Mchango wa marehemu Augustine Mahiga kwa mfano katika kuleta amani nchini Somalia. Yawezekama Wasomali wakamkumbuka kuliko sisi Watanzania.

Watu kama Profesa Anna Tibaijuka katika medani ya kimataifa, tunakumbuka vipi mchango wake? Tunamwekea kumbukumbu gani hata kama ni ya strabe? Jaji James Bwana, ambaye alipata kuongoza nchi huko nje, tunamkumbuka vipi?

Si siri, kwamba kuna Watanzania wamefanya makubwa kitaifa na kimataifa, lakini wanapokuwa wameondoka madarakani au kufariki dunia, huondoka na kila kitu chao na kubaki wa kawaida na hata kusahaulika kabisa.

Bila shaka, ipo wizara kama si idara, ambayo inaweza kufuatilia michango ya Watanzania mmoja mmoja au kwa vikundi ndani na nje ya nchi na kuratibu jinsi ya kuwakumbuka kutokana na michango yao katika Taifa. Tunaweza kuwa na madaraja kama ya Mfugale mengi tu.

Bado tunaweza kuwa na majengo kama ya Mkapa kwa idadi kubwa tu, viwanja kama vya Abeid Kaluta vingi tu, barabara kama za Sophia Kawawa nyingi tu, au hata viwanja vya Abeid Amani Karume vingi tu, kama kumbukumbu za Watanzania wenzetu waliotoa michango iliyotukuka kwa Taifa na kwa Watanzania.

Tusiache watu wetu mashuhuri waondoke na michango yao ipotee bila kuwaachia kumbukumbu, hususan katika kipindi hiki ambacho Rais John Magufuli ameagiza somo la Historia kuwa la lazima katika shule zetu. Tutasomaje Historia bila kukumbuka michango ya watu wetu? Alamsiki!

UCHUMI

# Tarime yawekeza uchumi katika majengo yatakayoingiza mamilioni kodi, ajira kibao



Sehemu ya jengo la vibanda 63 vya maduka ya biashara ya kitega uchumi cha Halmashauri ya Mji wa Tarime, lililojengwa kwa mkataba na mwekezaji wa ndani. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

**Na Anthony Gervas,** aliyekuwa TARIME

ALHAMISI wiki iliyopita, kulikuwapo simulizi za Halmashauri ya Mji wa Tarime mkoani Mara, kujikita katika maboresho ya kituo cha afya, mahali kulikuwapo malalamiko kwao.

Hiyo ni sekta moja, maana katika nyanja ya uchumi nako si haba wameamua kuwekeza. Hapo ndipo kunapatikana mradi wao jengo la kitega uchumi, kuwapo vibanda 63 vya maduka ya biashara katika eneo la soko la Rebu mjini hapa, uliojengwa kwa ubia mwekezaji binafsi mjini hapa, Charles Mwita.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji huo, Elias Ntiruhungwa, anayefafanua kwamba: "Tumeingia ubia na mwekezaji binafsi wa ndani atakayeendesha kwa mkataba wa miaka 15."

Kwa mujibu wa mkurugenzi ni kwamba, baada ya mwekezaji huyo kukamilisha miaka hiyo ya ubia, katika maarajio ya kurejesha gharama zake za ujenzi na faida, mradi utarejeshwa kwa halmashauri hiyo.

Anataja gharama kuu ni jumla ya Sh. 233,602,000 kwa ujenzi huo ulioanza Agosti mwaka jana na uko hatua za mwisho kukamilika, ukilenga kuwanufaisha wananchi wa Tarime kibiashara na kiuchumi,

### MANUFAA YALIYOPO

Anafafanua manufaa yaliyoko ni wakazi wa mji huo kufanya biashara, kuajiriwa, kumiliki mitaji ya biashara, kujiongezea kipato wao na halmashauri yenyewe.

Mkurugenzi huyo anataja matarajio ya mapato ni wastani wa kodi Sh. milioni 30.240 zitakazokusanywa kwenye vibanda kila mwaka.

Pia, anataja pato la ushuru kwa

> **"Hadi sasa kuna utekelezaji miradi iliyofikia asilimia 50 na mingine asillimia 95, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo kupaua na kuweka nondo, madirisha, milango na kupaka rangi.**



Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Belton Garigo akiwa ofisini kwake mjini Tarime.

huduma zitolewazo kila mwaka, akifafanua kuwapo mapato ya serikali kuu kupitia ushuru na tozo mbalimbali, pia wastani wa Sh. 6,300,000 zitakazokusanywa kupitia ada ya leseni na ushuru wa mwaka.

Ntiruhungwa anataja faida nyingine, ni kuongeza huduma kwa wananchi wa mji Tarime na wengine wanaofika kutoka sehemu mbalimbali na kuboresha muonekano wa mji huo.

### MAKAO MAKUU

Mradi mwingine ni jengo la ghorofa la makao makuu, ambayo Halmashauri ya Mji imeanza kujenga tangu mwaka juzi na unatarajiwa kukamilika mwaka ujao.

Mradi huo umepangwa kuchukua siku 1,042 sawa miaka miwili na miezi isiyopungua 10 na hadi sasa Mkurugenzi wa Halmashauri anasema umeshakamilika kwa asilimia 90, zawadi ya awali kiuchumi kwa wakazi ni kwamba imewazalishia ajira ya muda.

Ntiruhungwa anasema, kukamilika kwa mradi huo kutawapa watumishi mazingira bora ya kufanya kazi, kuongeza kima cha uchumi wa Tarime na mafundi wazawa wanaendelea kupata fursa ya kubadilisha ujuzi na wageni, wajenzi wa mradi.

Chanzo cha mapato ya ujenzi, mkurugenzi anasema Halmashauri ya Tarime imepokea msaada wa Sh. milioni 400 mgodi wa dhahabu wa North Mara na Sh.167 221,100, zilitengwa kwa ajili ya kujenga nyumba tatu za watumishi.

### MTAJI WA ELIMU

Katika elimu, anasema Halmashauri ya Mji Tarime imepata Sh. 968,778,222 kutoka serikali kuu kupitia mradi anaouita EP4R, kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Wavulana Tarime.

Anaeleza, utekelezaji wa mradi huo unagusa ukarabati na uwekaji miundombinu ya umeme, kupakaa rangi ndani na nje ya majengo na kuondoa milango na madirisha yaliyoharibika.

Mkurugenzi anaeleza imani yao viongozi kwamba ni maboresho yatakayoleta tija inayoongeza ufaulu wa wanafunzi, hadhi ya elimu Tarime, ufanisi na ni kutimiza majukumu yao kwa wakazi kwa ujumla.

Anataja faida zingine ni kusaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza,walimu kuongeza udahili wa wanafunzi na shule hiyo kuwa mazingira bora ya kujifunza.

Kinachofanyika pia, kinahusu ujenzi wa vyumba 16 vya madarasa na matundu 47 ya vyoo katika shule za msingi Turwa, Tagota, Sabasaba, Mtingiro, Nkongore, Azimio na Shule ya Sekondari ya Wavulana Nyamisangura, kupitia ufadhili wa fedha za EP4R, kiasi cha Sh.385, 100,000.

Anasema kuwa pia kuna ukamilishaji wa miradi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule za msingi nyagesese, mwibari, mtingiro na nyamwino uliogharimu kiasi cha Sh.56,664,901 kukamilika.

Mkurugenzi anasema, hadi sasa kuna utekelezaji miradi iliyofikia asilimia 50 na mingine asillimia 95, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo kupaua na kuweka nondo, madirisha, milango na kupaka rangi.

Ntiruhungwa anasema, miradi hiyo itakapokamilika itaongeza ufanisi wa ufundishaji na kujifunza, walimu na wanafunzi kupunguza utoro shuleni na mlundikano wa wanafunzi darasani na kupunguza kutembea umbali mrefu hadi shuleni.

Walimu nao wana manufaa si haba, Halmashauri ya Tarime imeshapokea Sh. milioni 50 kutoka serikali kuu kwa ajili ya kujenga nyumba mbili za walimu katika shule za msingi Mturu na Kemairi, ambazo hadi sasa umeshakamilika na matarajio ni kuondoa kero ya walimu kutembea umbali mrefu mtaani, huku ulinzi na usalama ukiimarishwa shuleni.

Hata hivyo, wakati wa utekelezaji miradi nao kumeshuhudiwa mengi, zipo shida katika miradi ya ujenzi kama vile kupanda bei ya vifaa vya ujenzi.

"Changamoto nyingi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali zimekuwa zikijitokeza, hivyo kusababisha hata mradi wetu wa ujenzi wa jengo la utawala kusimama, mkandarasi wa ujenzi kutozingatia muda wa mkataba ambaye ni Wakala wa Majengo (TBA)," anasema.

Ni hali inayosababisha mradi huo kukwama na kwamba ufinyu wa bajeti ya fedha kutoka serikalini, nao ni moja wapo ya sababu zina zokwamisha kukamilika miradi.



# Mpango mkakati afya, usafi mazingira waja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kuzindua Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Afya na Usafi wa Mazingira (2021-25).

Mpango Mkakati huo unalenga kuimarisha huduma za afya ya usafi mazingira ili kukabiliana na milipuko ya magonjwa yatokanayo na usafi duni, ikiwamo kipindupindu, kuhara na kichocho.

Pamoja na mambo mengine, Mkakati huo unalenga kutengeneza mfumo wa kuziwezesha Wizara na Taasisi husika kufanya kazi kwa pamoja katika kuboresha usafi wa afya ya mazingira.

Wizara hizo ni Elimu, Maji, Ofisi ya Raisi (TAMISEMI), Mamlaka ya Dawa na Vifaa vya Tiba Tanzania (TMDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Mkakati huo unatarajiwa kuzinduliwa leo jijini Dodoma na Waziri wa Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Doroth Gwajima, katika kilele cha mkutano wa mwaka wa Afya na Usafi wa Mazingira unaofanyika jijini hapa kwa siku nne.

Katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Mabula Nchembe, alisisitiza kuwa afya na usafi wa mazingira ni eneo nyeti kwani inahusika na afya ya kisaikolojia, akili na afya ya binadamu.

Prof. Nchembe aliwataka washiriki wa mkutano huo kuzingatia weledi na maadili yao katika kutekeleza shuguli zao za kila siku.

"Mnakabiliwa na jukumu kubwa na changamoto kwani katika ofisi nyingi, maeneo ya umma, na mashule ndani ya nchi hali ya afya na usafi wa mazingira bado sio nzuri.

Lazima ninyi wenyewe muonyeshe maana ya usafi wa mazingira," aliwapa changamoto maofisa wa afya wa mazingira.

Aliwaonya baadhi ya maofisa wa afya na usafi wa mazingira ambao wanaendekeza tabia mbaya ya kupokea rushwa ili wasikague katika baadhi ya maeneo, ambayo hayatekelezi matakwa ya usafi wa mazingira.

Pia, alizungumzia juu ya hitaji la kuanzisha na kutekeleza utaratibu mzuri wa kufuatilia na kuondoa kwa wakati taka vifaa vikali vinavyozalishwa kutoka hospitali na vituo vingine vya huduma za afya.

"Inasikitisha sana na ni hatari kwamba katika maeneo mengi vifaa vilivyotumiwa hospitalini na katika vituo vya afya vinazagaa katika mitaa mbalimbali, hali ambayo inahatarisha afya ya jamii," alisema

Mkurugenzi Msaidizi, Afya ya Mazingira na Usafi wa Mazingira, wizara hiyo, Dk. Khalid



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Water Mission Tanzania, Benjamin Filskov, wakikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa mradi wa maji wa Msamalo wilayani Chamwino-Dodoma. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lawakomboa wakazi 4,000 adha ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIDA ya maji kwa Wakazi wa Kata ya Msamalo, Chamwino mkoani Dodoma itabaki kuwa historia baada ya kuzinduliwa kwa mradi wa maji utakaowanufaisha zaidi ya wakazi 4,000 na taasisi za kijamii.

Katika kuhakikisha watu wengi wanafikiwa na huduma ya majisafi na salama, Shirika la Water Mission Tanzania kwa kushirikiana na serikali kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), limezindua mradi huo ambao utapunguza adha ya kufuata maji umbali mrefu kwa wakazi 4,085 wa eneo hilo.

Pia mradi huo utazinufaisha zaidi ya kaya 730 na taasisi mbalimbali za kijamii zikiwamo zahanati, masoko na zile za kidini jambo ambalo linaashiria ustawi wa watu na shughuli za kijamii na kiuchumi.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano, Mkurugenzi Mkazi wa Water Mission Tanzania, Benjamin Filskov, alisema utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya mkakati wa shirika katika kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata majisafi na salama karibu na makazi yao.

Filskov alisema lengo la mradi huo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na mfumo thabiti wa kupata majisafi na salama karibu na makazi yao.

"Tunatambua uwapo wa mahitaji makubwa ya maji kwenye eneo hili na leo hii tunayo furaha kuzindua mradi huu ambao utasaidia kupunguza adha ya maji kwa wakazi wa eneo hili. Mafanikio haya ni ishara ya ushirikiano wetu na RUWASA na Wizara ya Maji katika kusaidia jitihada za serikali kufikisha huduma za maji kwa watu wote," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandishi Antony Sanga, alisema kukamilika kwa mradi huo ni utekelezaji wa ahadi za serikali katika kupunguza kero ya maji kwa wananchi na kwamba utasaidia kuboresha maisha ya wakazi wa eneo hilo.

"Tunamshukuru sana Rais wetu, wakati wa kampeni aliahidi kwamba tutawapelekea wananchi wetu huduma ya maji hivyo huu ni upendo wake kwenu wana Msamalo," alisema.

Aliwataka wakazi wa Msamalo kushirikiana ili kuendeleza mradi huo ili uwe endelevu kwa manufaa kwa vizazi vijavyo.

Mradi huo unatumia nishati ya jua 'Solar' ambapo maji yanavutwa kutoka kwenye kisima na kwenda kwenye kituo cha kusafisha na kutibu maji na baadaye yanapelekwa kwenye vituo 18 vilivyoko karibu na makazi ya watu.

# Mapato ya utalii yapaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, amesema mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 7.9 kutoka Dola za Marekani milioni 2,412.3 mwaka 2018 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,604.5 mwaka 2019.

Dk. Nzuki aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipowasilisha matokeo ya utafiti wa hali ya utalii nchini mwaka 2019.

"Utalii umeendelea kuwa ni shughuli muhimu katika uchumi wa Tanzania na ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi zaidi nchini," alisema.

Dk. Nzuki alisema takwimu zinaonyesha idadi ya watalii iliongezeka kutoka watalii 1,505,702 mwaka 2018 hadi 1,527,230 mwaka 2019.

Alifafanua kuwa mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yametokana na jitihada za serikali kwenye uwekezaji na utangazaji wa Tanzania kama eneo lenye vivutio vya kipekee vya utalii.

"Katika kutambua umuhimu wa sekta ya utalii katika uchumi wa taifa, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii Zanzibar, imekuwa ikifanya utafiti wa watalii wanaoondoka nchini kila mwaka," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema mkutano wa watendaji wakuu uliofanyika juzi, ulipitia na kuwasilisha matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2019.

Alisema matokeo hayo yanaonyesha wastani wa matumizi ya watalii kwa siku uliongezeka kutoka Dola za Marekani 193 mwaka 2018 hadi kufikia Dola za Marekani 266 mwaka 2019.

"Watalii walionunua huduma kwa njia ya vifurushi kwa mwaka 2019 walitumia wastani wa Dola za Marekani 379 kwa mtalii kwa siku kulinganishwa na Dola za Marekani 331 mwaka 2018," alibainisha.

Dk. Nzuki alisema watalii ambao hawakununua huduma kwa vifurushi, walitumia wastani wa Dola za Marekani 216 kwa mtalii kwa siku mwaka 2019 kulinganishwa na Dola za Marekani 135 mwaka 2018.

Pia, alisema utafiti huo unaonyesha gharama za kutalii nchini hazipishani sana na za nchi jirani, na idadi kubwa ya watalii walitoka nchi za Marekani, Uingereza na Ujerumani katika kipindi cha mwaka 2019.

"Utafiti huu pia unaonyesha asilimia 67 ya watalii walikuja kwa ajili ya mapumziko na burudani na shughuli za utalii zilizovutia wageni wengi ni wanyamapori, utalii wa fukwe na kupanda mlima," alifafanua.

Alisema kwa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara, Tanzania inashika nafasi ya pili kwa kuingiza fedha za kigeni kupitia sekta hiyo baada ya kinara nchi ya Afrika ya Kusini.

Alisema moja ya kero ambazo zimebainishwa na watalii ni miundombinu hafifu na matumizi ya kiwango cha chini sana ya Credit card.

"Hivi sasa watu wanaotembea na fedha taslimu wanapungua sana, watu wengi wanatumia sana kadi, sasa hili inabidi tuliangalie ili kuona tatizo lipo wapi kama ni mifumo au wadau ndiyo hawataki kutumia," aliagiza.



## 50 mbaroni madai utoroshaji madini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watu 50 wamekamatwa na polisi katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kutokana na sakata la utoroshaji wa madini lililoibuka hivi karibuni na kusababisha Waziri wa Madini, Dotto Biteko kuwachukulia hatua baadhi ya maofisa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watu waliokamatwa ni mawakala wa ununuzi wa dhahabu, wafanyabiashara na baadhi ya maofisa wa Ofisi ya madini.

Alisema baada ya ziara ya Waziri zoezi la kuwasaka watu hao na kuwakamata watu hao kwa ajili ya hatua mbalimbali lilianza na ndipo watu hao wakakamatwa kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo.

"Kuna baadhi ya mambo hatuyasemi kwa sababu hili jambo ni la kiuchunguzi zaidi, tukiyasema kuna wengine wanaweza wakakimbia tukawa tumeharibu ushahidi, lakini hili zoezi lilianzishwa na Waziri mwenyewe," alisema Kamanda Matei.

Alisema kwenye sakata hilo baadhi ya watu wanaotuhumiwa zipo mamlaka zingine za kushughulika nao na wengine wanashughulikiwa kwenye ngazi ya kipolisi.

Mwanzoni mwa wiki hii, Waziri wa Madini Biteko, alifanya ziara wilayani humo na akachukua hatua mbalimbali dhidi ya watu ikiwamo kumtumbua Mwenyekiti wa Soko la Madini la Chunya pamoja na kuwasimamisha kazi watumishi watatu wa ofisi ya madini ya mkoa huo wa kimadini.

Alifuta leseni saba za wanunuzi wa dhahabu wilayani humo na akaagiza mawakala 13 wa ununuzi wa dhahabu kujisalimisha wenyewe polisi.

"Naagiza pia maeneo yote ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia mercury (mialo) yasajiliwe ili iwe rahisi kudhibiti dhahabu inayopatikana huko isitoroshwe," alisema Biteko.

Baada ya Waziri Biteko kutoa maagizo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alianza utekelezaji kwa kumtaka Kamanda Matei kuwakamata wote waliotajwa na Waziri.

"Naagiza RPC uanze utekelezaji mara moja, hawa watumishi watatu pamoja na Mwenyekiti wa Soko la Madini wakamatwe na kuwekwa ndani ili wakahojiwe wakiwa ndani, pia hata wale 13 ambao Waziri ameagiza wakajisalimishe wenyewe Polisi wasihangaike kwenda Polisi, wala wasitumie mafuta yao kwenye magari kwenda Polisi mimi naagiza Polisi wakawakamate huko huko walipo," alisema Chalamila.

# Mtoto aliyeibwa ailiza mahakama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI, mashahidi na baadhi ya maofisa waliokuwa ndani ya ukumbi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbeya, wamejikuta wakimwaga machozi, baada ya mtoto aliyeibwa kuingia ndani ya ukumbi huo kwa lengo la kutoa ushahidi kuanza kulia baada ya kumuona mtuhumiwa.

Hali hiyo ilisababisha kesi hiyo ya wizi wa watoto kusimama kwa muda kupisha hali ya simanzi iliyokuwa imetawala mahakamani.

Kabla ya kuibuka vilio ndani ya mahakama hiyo, Hakimu wa Wilaya, Zawadi Laizer, alikuwa akiendelea kusikiliza kesi hiyo, ambapo ushahidi wa awali ulianza kutolewa na baba mzazi wa watoto hao ambao ni Faisal Mashaka (5) na Farhana Mashaka (2).

Watoto hao wanadaiwa waliibwa na Hawa Mhalipa, Disemba 28 mwaka jana katika eneo la Ituha jijini Mbeya na walipatikana Januari 2, mwaka huu katika Wilaya ya Nzega mkoani Tabora.

Baada ya baba mzazi wa watoto hao, Mashaka Juma kumaliza kutoa ushahidi, shahidi wa pili alikuwa ni mtoto Faisal, ambaye ni miongoni mwa watoto hao.

Hakimu Laizer alimwita kizimbani mtoto Faisali ili atoe ushahidi wake na mtoto akaitika na kujongea kuelekea mahali kilipo kizimba cha mashahidi.

Hata hivyo, baada ya kuingia kizimbani na kutulia ili aanze kuieleza mahakama ushahidi wake, aliinua macho na kutazamana ana kwa ana na Hawa (mtuhumiwa) na ndipo alianza kububujikwa na machozi, huku akionekana kujawa na hofu.

Kilio cha mtoto huyo kiliibua simanzi kwa watu waliokuwa ndani ya ukumbi wa mahakama, ambapo nao wakaanza kutokwa na machozi, hali iliyosababisha Hakimu Laizer kuahilisha kesi hiyo kwa muda.

"Kesi hii naiahilisha kwa muda ili mkamnyamazishe mtoto, askari mtoe kwanza nje mshtakiwa mpaka mtoto atakaponyamaza ndipo tutaendelea kusikiliza ushahidi," alisema Hakimu Laiser.

Baada ya maelezo hayo ya Hakimu, mama mzazi wa mtoto huyo pamoja na ndugu zake wengine walimchukua mtoto wakatoka naye nje ya mahakama ili kumnyamazisha na askari walimhamisha mshtakiwa kutoka alipokuwa amekaa na kumuweka mahali ambapo mtoto asingeweza kumuona.

Hali ya utulivu ilirejea na ndipo Hakimu Laizer akaruhusu Feisal kuendelea kutoa ushahidi wake, ambapo aliieleza mahakama kuwa mama huyo aliwachukua yeye na mdogo wake na akawaambia anawapeleka Mpanda mkoani Katavi.

Alisema baada ya kuondoka na mama huyo walikuwa wanaamini kuwa wanapelekwa Mpanda, lakini wakajikuta wapo mkoani Tabora, ambako walikuwa hawajawahi kufika. Hakimu Laiser alisema kesi hiyo imechelewa kwa sababu mshtakiwa Hawa alitakiwa apelekwe kwanza katika Hospitali ya Gereza la Isanga mkoani Dodoma ili akapimwe kama ana matatizo ya akili.

"Taratibu za kumpeleka Dodoma na kurudishwa ndizo zilizochelewesha kesi hii, lakini baada ya kupimwa ilibainika kuwa ana matatizo ya akili ambayo yanamfanya wakati mwingine asiweze kujieleza kabisa," alisema Hakimu Laizer.

Hata hivyo Kesi hiyo iliahirishwa hadi Disemba 24, mwaka huu ambapo mashahidi wengine wataendelea kusikilizwa. Mshtakiwa alirudishwa rumande.



Maofisa wa kampuni ya uwekezaji wa pamoja (UTT AMIS), wakikata utepe kuashiria ufunguzi wa kituo cha kuhudumia wawekezaji wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Tulia awapa neno wasambazaji wa gesi ya kupikia majumbani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA.

KAMPUNI zinazosambaza gesi ya kupikia majumbani, zimeshauriwa kufikisha huduma hiyo hadi maeneo ya vijijini ili wananchi waitumie na kuachana na matumizi ya nishati za kuni na mkaa ambazo zinaathiri mazingira.

Wito huo ulitolewa juzi na Mbunge wa Mbeya Mjini, ambaye pia ni Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, wakati akizindua kituo cha kujaza mitungi ya gesi ambacho kimefunguliwa na kampuni ya Orxy jijini Mbeya. Dk. Tulia alisema wananchi walio vijijini wanatumia zaidi nishati za kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia kwa vile huduma ya gesi ya kupikia haiwafikii na baadhi yao hawana elimu ya matumizi sahihi ya kupikia gesi.

"Umefika wakati ambao kampuni zinazosambaza gesi ya kupikia majumbani mpanue huduma zenu ziende hadi kwa wananchi wanaoishi vijijini ili na wao waachane na matumizi ya kuni na mkaa," alisema Dk. Tulia.

Alisema matumizi ya gesi yatawasaidia wananchi hasa wanawake kuokoa muda mwingi wanaoutumia kuandaa vyakula, huku pia wakiachana na kukata miti hovyo, hivyo kutoharibu mazingira.

Dk. Tulia alipendekeza kuwa ili gesi hiyo iwafikie wananchi hadi vijijini wauzaji wa bidhaa hiyo wanapaswa kupunguza bei ili nishati hiyo iwe nafuu kuliko kuni na mkaa. Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya gesi ya Oryx, Benedict Araman, alisema kampuni hiyo inaendelea kupanua uwekezaji katika sekta ya gesi sambamba na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi salama ya gesi.

Araman alisema baadhi ya wananchi wanaogopa kutumia gesi kwa kupikia wakiamini ni hatari na sasa kampuni hiyo inafanya kazi ya kuwaelimisha namna ya kuitumia bila kuwaletea madhara.

Baadhi ya mawakala wa usambaji wa gesi mkoani Mbeya walisema uwapo wa kituo cha kujaza mitungi ya gesi mkoani Mbeya utasaidia gesi hiyo kupatikana kirahisi kwa watumiaji.

Amoud Said, muuzaji wa mitungi ya gesi jijini Mbeya, alisema kituo hicho kitawapunguzia gharama ya kusafirisha mitungi iliyojaa gesi kutoka Dar es Salaam kisha kuirejesha baada ya matumizi ili ijazwe tena, hali ambayo itasaidia hata bei ya mitungi ya gesi kupungua.





Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, akimfariji mtoto Sabaha Maulid Juma, aliyeunguzwa mafuta ya moto na mama yake mzazi ambaye amelazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya matibabu. **PICHA NA RAHMA SULEIMAN**

# Hemed acharukia mashine ya maabara kutofanya kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kufuatilia makubaliano yaliyopo kati ya Kampuni ya Pyramid ya Dar es Salaam na taasisi ya Hipsi ya Zanzibar kuhusu usimamizi wa mashine maalum ya uchunguzi wa maabara.

Mashine hiyo iliwekwa kutoa huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini 'A' iliyopo Kivunge.

Agizo hilo alililitoa wakati wa ziara ya ghafla katika hospitali hiyo kuangalia uwajibikaji wa watendaji pamoja na huduma za afya wanazopata wananchi na kugundua mashine hiyo kutofanya kazi.

Hali hiyo inatokana na kuungua kwa taa ikiwa bado kwenye dhamana ya kampuni hiyo.

Alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya Hipsi iliyoshirikiana na kampuni Pyramid kutoa mrejesho wa taarifa na kupelekewa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini na baadae kuwasilishwa kwake kwa hatua zaidi.

Hemed alisema licha ya kwamba taifa limekuwa likipokea misaada na baadhi ya michango kutoka kwa washirika wa maendeleo na taasisi za kitaifa na kimataifa kwa ajili ya huduma za jamii, lakini Serikali haitakubali kuona wananchi wake wanaendelea kukosa huduma za afya kwa dharau ya mtendaji mmoja

Alisema Serikali italazimika kufuatilia mazingira halisi ya huduma za maabara za hospitali hiyo na pale itakapohisi kwamba waliopewa jukumu la kutoa huduma hizo hawako makini, haitasita kuachana nao badala yake italazimika kununua mashine zingine.

Akizungumzia huduma ya damu salama, Makamu wa Pili wa Rais aliwataka watendaji wa kitengo cha damu salama kwenye Hospitali hiyo ya Wilaya kutobweteka kwa kusubiri wananchi kuchangia huduma hiyo inayohitaji elimu na uhamasishaji mkubwa.

Hemed alisema watendaji wa kitengo hicho wanapaswa kutoa taarifa kwa wakuu wa wilaya na Mkoa na tayari wana uzoefu mkubwa katika shughuli za uhamasishaji wa uchangiaji damu wakizitekeleza kila mwaka.

Alisema inasikitisha kuona kitengo cha damu salama cha Hospitali hiyo imekusanya uniti nne tangu kianze kutoa huduma mwezi mmoja uliopita, wakati hata robo ya mahitaji halisi ya matumizi ya huduma hiyo kwa wagonjwa haijakidhi.

Hemed alisema matatizo wanayokumbana nayo wananchi wakati wa huduma za afya ikiwamo ukosefu wa dawa wanazoandikiwa na madakatari zitatafutiwa njia ya kuziondosha kwa kuwa Serikali inaendelea na sera zake za kutoa matibabu bure.

Naye Daktari Dhamana wa Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini 'A', Dk. Tamimu Said Hamad, alisema huduma za afya katika zimeimarika kiasi kwamba hata malalamiko ya baadhi ya wagonjwa yanaendelea kupungua.

Dk. Tamimu alisema zipo changamoto za kubanduka kwa dari na kupasuka kwa baadhi ya kuta na vyumba vya jengo jipya la hospitali hiyo, jambo linalowatia hofu hasa kwenye vyumba wanavyolazwa wagonjwa.

Baadhi ya wananchi waliofika kupata huduma za afya hosptalini hapo waliishauri Serikali kuendelea kufuatilia huduma za afya zinazotolewa na baadhi ya hospitali, kwa kuwa wapo baadhi ya watendaji wanaendelea kuwasumbuwa wagonjwa.

# RC awaonya masheha kuhusu rushwa

**Na Rahma Suleiman ,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, amesema kitendo cha kupokea rushwa kwa ajili ya kuhalalisha matumizi ya ardhi kitapoteza uaminifu wa sheha aliyeaminiwa na serikali kuwa kiongozi wa wananchi katika eneo lake.

Akizungumza na masheha wa Mkoa huo kwa nyakati tofauti, alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya watu wenye tamaa ya kuhodhi maeneo mengi ya ardhi kinyume cha sharia na taratibu, huku wakiwatumia masheha kuwahalalishia umiliki wa ardhi kwa kutoa rushwa.

Mustafa aliwatahadharisha viongozi hao wa shehia kutojiingiza katika vitendo hivyo, badala yake wazingatie maadili ya uongozi yanavyoelekeza na kutunza siri za serikali.

"Nawasihi sana masheha, lazima tubadilike na tuzingatie maadili ya dhamana zetu, tufanye kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi hasa katika matumizi bora ya ardhi, na tuendane na kasi ya serikali ya awamu ya nane kwa kufanya kazi," alisema Mustafa.

Aidha, aliwataka masheha kuweka utaratibu maalum wa kusikiliza maoni na shida za wananchi katika shehia zao na kujipangia mipango kazi itakayosaidia kuibua miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

"Masheha sasa lazima tuwe na ushindani katika shehia zetu kwa kuibua miradi ya maendeleo na kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwenye maeneo yetu na kutoa ajira kwa wananchi," alisema.

Akizungumzia suala la ulinzi na usalama, Mkuu huyo wa Mkoa aliwaagiza masheha kuhakikisha wanatoa taarifa ya baadhi ya watu wanaofanya vitendo vya ufunjivu wa amani katika maeneo yao ili wachukuliwe hatua.

"Masheha lazima tuhakikishe wananchi wanaishi bila ya hofu katika mitaa yetu, haiwezekani vijana wanatishia watu amani na sisi serikali tunawatizama tu...masheha tuache muhali, tuwafichue hao vijana ili tuimarishe ustawi wa jamii,'alisema.

Masheha hao walimuomba uongozi wa mkoa kuwasaidia kutatua changamoto za muda mrefu zinazowakabili katika shehia zao, ikiwamo migogoro ya ardhi.

Wakizungumza katika mkutano huo wakuu wa wilaya ya Mjini walimuhakikishia mkuu wa mkoa kuwa wataendelea kuwaongoza na kuwaelekeza vyema viongozi hao wa shehia ili kuendana na matakwa na kasi ya serikali ya awamu ya nane katika kuwatumikia wananchi.

# Washauriwa kuhamasisha kulima mwani

**Na Rahma Suleimman,**
ZANZIBAR

WANAWAKE wanaojishughulisha na kilimo cha mwani Zanzibar, wametakiwa kuwahamasisha watoto na ndugu zao wa kiume kulima zao hilo ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya wakufunzi wa wakulima wa mwani yanayoendelea kwenye Wawi Mkoa wa Kusini Pemba, aliekuwa Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema si busara kukiona kilimo hicho kuwa ni kwa ajili ya wanawake peke yao.

Alieleza kuwa kilimo cha mwani kina faida kubwa kama kitafanywa kitaalamu na pia kina nafasi kubwa ya kubadilisha maisha ya wananchi, wakiwamo wanaume na kuinua pato la taifa.

Aidha, aliwaomba kinamama wanaolima mwani, wawahamasishe watoto wao wa kiume kujiunga na mafunzo ya kilimo hicho badala ya kuendekeza kukaa vijiweni.

Balozi Amina alisema iwapo wanaume watachangamkia kilimo cha mwani, watahukua nafasi za wazazi wao kwa kuwa utafika wakati hawatakuwa na nguvu za kuendesha shughuli za uzalishaji.

Alibainisha kuwa wakati Serikali ya Zanzibar ikianza mkakati wa kuimarisha uchumi wa buluu, ni wajibu kwa wananchi wote kuiunga mkono kwa kushiriki kwa vitendo kwenye uzalishaji wa rasilimali zitokanazo na bahari.

Wakufunzi 30 wanaoshiriki mafunzo hayo kutoka maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba, waliishukuru Taasisi ya REPOA iliyoandaa warsha hiyo, wakisema fursa hiyo itawapa mbinu za kitaalamu za kulima mwani katika maji ya kina kirefu sambamba na kuzalisha kwa wingi na kiwango bora kinachokubalika kwenye soko la kimataifa.

Naye Mtafiti Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Sera za Maendeleo na Umasikini (REPOA), Steven Mombela, alisema taasisi hiyo imebaini changamoto kadhaa zinazowakabili wakulima wa mwani, hivyo wamejidhatiti kuleta mapinduzi kwa kuwaendeleza wakulima wa zao hilo kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuwapa njia sahihi za kuimarisha ubora.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676


## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KENNEDY ELIBARIKI JACKSON** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T.575 CVR** chasis namba **SR4001106**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**WMB/RB/1220/2020**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**KATIKA BARAZA LA ARHDI NA NYUMBA LA WILAYA MASWA**
**MAHALI MASWA**
**MAOMBI NAMBA 71 YA MWAKA 2020**
**KATI YA**
**EMMANUEL SENI BUNDU............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. **JINUMBU JISENA**
2. **SAYI SENI**
3. **NJILE SENI.......................WAJIBU MAOMBI**

**WITO / TAARIFA**
**Kwa: NJILE SENI POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi dhidi yenu, katika Baraza hili la wilaya ya Maswa. Maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani. Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi **(WSD)** kabla ya tarehe **4.01.2021.** Pia unajulishwa kuwa maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya **tarehe 4.1.2021 saa 2:30** asubuhi mbele ya **Mhe. J.F.** Kanyerinyeri Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya – Maswa. Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakaidi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako. **IMETOLEWA kwa MKONO** wangu na **MHURI** wa Baraza hili leo **Tarehe 26.11.2020.**

## APARTMENT INAPANGISHWA

Ilala Bungoni, ground floor, meta 100 kutoka barabara kuu, ina vyumba vitatu, sebule, sehemu ya chakula, jiko, choo, ipo ndani ya fensi. Inafaa kwa ofisi, hostel ya wanafunzi. Kodi 500,000/= kwa mwezi.
**Simu; 0772 395249**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DAUDI V BONDA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC506CBH** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa CONTROL NUMBER **9910819940397**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ESTHER LYMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0353-0005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **PARANE SEKONDARI** mwaka 1996. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/865905/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFREY RWEHUMBIZA NJUNWAS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 655 BKV** TOYOTA SALOON. Chassis namba **NCP300022898.** Engine namba **2NZ1695832.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DSM/PHQ/RB/863142/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHANI JUMA MBONDELA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC838BUX**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa CONTROL **NUMBER 9910819940191**


OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
P.O.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

*Uza,*
*Chenye Thamani*
*Kubwa Kwa Kutangaza*
*Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
P.O.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Ataka kipaumbele makandarasi wazawa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeiagiza kamati maalum iliyoundwa na kuratibiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ambayo ndani yumo Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), kuhakikisha wanaangalia miradi ambayo itatumika kuwafundishia makandarasi wazawa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi anayeshughulikia sekta ya ujenzi, Msanifu Majengo, Elius Mwakalinga, alisema yako malalamiko ya baadhi ya makandarasi wazawa kuwa wamekuwa wakinyimwa kazi kauli ambayo aliikanusha si cha kweli.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika kikao cha tatu na cha kwanza cha mwaka 2020/25 cha baraza hilo kilichojumuisha pia Chama cha Wafanyakazi wa Ujenzi (TAMICO) Wilaya na Mkoa, alisema kupitia miradi huyo itawawezesha makandarasi hao kujengewa uwezo.

"Kamati iliyoundwa ikiratibiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) iende kwenye taasisi zilizopo chini ya sekta ya ujenzi wakachukue mpango wa manunuzi ili kuona kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21.

"Waangalie miradi yote ambayo imeainishwa inatekelezwa katika kipindi cha bajeti ya mwaka huu wa fedha, katika miradi hiyo, waangalie ipi inafaa kuwafundishia wazawa," alisema.

Mwakalinga alisema ile ambayo wanaiona inafaa waanze kuwafundishia makandarasi wazawa ili nao washindanishwe wakae sawa.

Kuhusu NCC, Mwakalinga alisema matarajio ya serikali na Watanzania ni kwamba baraza hilo, litoe miongozo ya gharama za ujenzi kwa wakati na kwa usahihi ili zitumike katika miradi mbalimbali inayotekelezwa.

Aliwaeleza watendaji wa baraza hilo kuwa hawawezi kutoa gharama za ujenzi kama watu wao hawajui vifaa vinatolewa wapi na gharama zake bila kuenda eneo husika mradi unakotekelezwa.

Pia alisema migogoro ndiyo inayoua miradi na kuwataka watafute suluhu mapema kabla haijatokea.

"Migogoro ni jambo baya inayoua miradi, kama kuna mahali mnasikia inataka kutokea nendeni mkaisuluhishe, ongezeni mwendo wa kuitatua migogoro ili isitokee, tena msiogope kuitwa wanoko," aliwaeleza.

Awali, Mtendaji Mkuu wa NCC, Dk. Matiko Mturi, alisema baraza hilo lilianzishwa mwaka 2018/19 na kikao cha kwanza kilikuwa Februari, mwaka jana na cha pili kilifanyika kwa siku mbili mwanzoni mwa mwaka huu.

# Bandari ya D'Salaam yairidhisha Rwanda

**Na Mwandishi Wetu**

RWANDA imeeleza kuridhishwa na huduma zinazotolewa katika Bandari ya Dar es Salaam, ambayo inahudumia zaidi ya asilimia 80 ya mizigo ya nchi hiyo na kuahidi kuendelea kuitumia.

Balozi wa Rwanda nchini, Meja Jenerali Charles Karamba, aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi. Balozi Karamba alisema nchi yake itaendelea kuitumia bandari hiyo kupitisha mizigo yake.

"Tanzania na Rwanda siyo nchi jirani pekee, bali ni ndugu wa damu, Rwanda inaiona Bandari ya Dar es Salaam kama Bandari ya Rwanda," alisema.

Naye Waziri Prof. Kabudi alisema Tanzania itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara kwa nchi jirani na nyingine zinazoitegemea kupokea na kusafirisha mizigo yake.

"Tanzania imekuwa ikitumia ndege za Rwanda kusafirisha minofu ya samaki nje ya nchi, wakati tukijipanga kununua za kwetu ili kuongeza kasi ya biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki," alisema.

Katika mazungumzo hayo pia, Balozi Meja Jenerali Karamba alitumia fursa hiyo kumfahamisha Prof. Kabudi kuhusu uwapo wa mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya za Madola unaotarajiwa kufanyika Juni mwaka huu nchini humo.

Alisema hiyo itakuwa fursa nzuri zaidi kwa wafanyabiashara wa Tanzania na Rwanda kufanya biashara kutokana na uwapo wa mkutano huo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya Musoma, mkoani Mara, Tanna Nyabange, akizungumza jana na wavuvi wa Busekera, kwenye ziara ya kuwahamasisha wajiunge katika vikundi, ili waweze kupata mikopo ya halmashauri na taasisi nyingine za fedha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Ajali basi yaua mtoto, yajeruhi 23

**Na Neema Sawaka,** MWANZA

MTOTO asiyefahamika anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka saba, amefariki dunia na wengine 23 kujeruhiwa katika ajali ya basi kampuni ya Frester linalofanya safari kati ya Kahama na Musoma.

Ajali hiyo iliyohusisha basi lenye namba za usajili T 965 DST, ilitokea jana majira ya saa 12:00 asubuhi muda mfupi baada ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mutafungwa, kulikagua katika kituo cha mabasi mjini Kahama.

Baada ya basi hilo kuruhusiwa, muda mfupi lilipata ajali eneo la Nyakato nje kidogo ya mji wa Kahama kutokana na mwendokasi. Kamanda Mtafungwa alisema basi hilo lilikuwa na abiria 47 na kwamba kati yao 23 walijeruhiwa na watatu kati yao hali si nzuri.

"Dereva huyu ni mzembe, haiwezekani upatiwe elimu ya usalama barabarani halafu muda huo huo ukiuke sheria na kusababisha ajali kwa uzembe, ambayo imesababisha ajali kwa watu 23 na kusababisha kifo cha mtoto mmoja. Tutachukua hatua kali dhidi yake pindi atakapokamatwa," alisema Mutafungwa.

Mmoja wa majeruhi hao, Cassian Msaki, alisema dereva wa basi hilo alikuwa anaendesha kwa mwendokasi na kwamba alipofika eneo la tukio, alishindwa kulimudu gari wakati akilikwepa gari dogo lililokuwa mbele yake, hivyo kuingia mtaroni na kupinduka.

"Dereva wa basi hili alikuwa anafanya mashindano na mabasi mengine. tunaomba serikali ichukue hatua kali dhidi yake," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alizitaka mamlaka zinazosimamia usalama barabarani kuhakikisha zinachukua hatua za kisheria kwa madereva ambao ni wazembe kwa kufungia leseni zao ili wajifunze.

"Haiwezekani tuendelee kuwavumilia madereva wa mabasi wanaoendelea kufanya mashindano barabarani, huku wakiwa na abiria, tutatuchua hatua kali kwao ili kudhibiti ajali zinazosababisha vifo kwa watu bila sababu na kupunguza nguvu kazi ya taifa," alisema Macha.

## Kesi ya Padri kuanza Januari 11

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, imepanga kusikiliza maelezo ya awali katika kesi inayomhusu Padri Erasmus Kessy, Januari 11, mwakani.

Kiongozi huyo anadaiwa kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi huyo aliyekuwa akisoma kidato cha nne (jina lake na shule vinahifadhiwa) kinyume cha kifungu namba 130 (1), (2) e cha Sheria ya Adhabu Sura 16 na marekebisho 2019.

Kesi hiyo namba 159 ya mwaka huu, ilitajwa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Thurston Kombe, ambaye alisema mshtakiwa huyo atasomewa maelezo ya awali Januari 11.

Awali, ilidaiwa mahakamani humo na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Lobulu Mbise, kuwa Machi, mwaka huu, katika hoteli moja iliyoko katika Mji wa Boman'gombe wilayani Hai kwa nyakati tofauti, Padre Swai alimbaka mwanafunzi huyo.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa alimpeleka katika hoteli moja na kukodi chumba na kumrubuni na baada ya miezi mitatu aligundulika kuwa na ujauzito ndipo shauri hilo lilipofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Hai.

# PIRLO AMTETEA RONALDO KWA KUKOSA PENALTI



**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo amemtetea Cristiano Ronaldo kwa kushindwa kufunga penalti na kusema mabingwa pia hukosa penalti, wakati Juventus ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na Atalanta kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie, Jumatano.

Penalti ya Ronaldo ya dakika ya 61 iliokolewa na golikipa wa Atalanta, Pierluigi Gollini na kuufanya mchezo huo kumalizika kwa sare ya 1-1 na kuwanyima pointi tatu mabingwa hao watetezi.

Federico Chiesa aliiweka mbele Juve kwa bao lake la daika ya 29 na likasawazishwa na Remo Freuler.

Wakati Chiesa alipodondoshwa chini na Hans Hateboer dakika nne baadae, mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo shuti lake la penalti liliokolewa kirahisi na golikipa Gollini.

Ronaldo sasa ameshindwa kufunga penalti nne kati ya 30 alizopata hapo kwa Bianconeri, lakini gwiji na kocha wa Juve, Pirlo hakusita kusifia mchango wa fowadi huyo.

"Haukuwa mchezo rahisi, lakini alifanya vizuri,"alisema Pirlo akiwaambia waandishi wa habari. "Kama angefunga penalti yake, kungekuwa na mitazamo tofauti kabisa.

"Alifanya kile alichotakiwa kukifanya, pengine haikuwa kawaida kama ilivyozoeleka, lakini yeye ni bingwa na mabingwa huwa wanakosa penalti pia."

# Solskjaer: Man Utd lazima iimarike

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anaamini mashetani wekundu hao wanaweza kuimarika "zaidi" ili kuwa miongoni mwa timu zitakazotoa changamoto kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

United wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi, wakipitwa pointi nane na vinara na bingwa mtetezi Liverpool, lakini wakiwa na michezo miwili, mmoja ukipigwa jana Alhamisi dhidi ya Sheffield United.

Mashetani wekundu hao msimu uliopita walimaliza Ligi wakiwa wamepitwa pointi 33, lakini Solskjaer haoni kama wameachwa mbali zaidi na kikosi cha Jurgen Klopp kwenye mbio za ubingwa.

Solskjaer amesisitiza mbio za ubingwa wa msimu huu 2020-21 bado ziko wazi, lakini akakubali kwamba, lazima wachezaji wake waongeze juhudi na kujituma.

"Hizi ni mbio kubwa kwa upande wetu," amesema Solskjaer.

"Nakatishwa tamaa kama wachezaji hawawezi kufikiria kwamba tunaweza kutoa changamoto kwa mbio za ubingwa.

"Kuna sababu tofauti kwa matokeo tofauti. Nahisi tunakuwa bora zaidi, lakini tunatakiwa kuimarika zaidi kwa ajili ya hatua inatofuata."





# Pioli achukizwa Milan kuruhusu mabao

**MILAN,** Italia

STEFANO Pioli anahisi AC Milan inaruhusu mabao mengi zaidi ya kufungwa, wakati wakitoka sare ya 2-2 na Genoa kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumatano.

Rossoneri hao walitoa sare ya 2-2 kwa mara ya pili wakati Davide Calabria na Pierre Kalulu walisawazisha mabao ya Mattia Destro.

Milan imeruhusu mabao 13 kwenye Serie A msimu huu na kocha Pioli anaona kwamba timu yake inatakiwa kuimarisha zaidi safu yake ya ulinzi kwa kuiambia DAZN: "Ni sare kwenye mchezo mgumu, kwenye dimba gumu.

"Tungeweza kupata uongozi kipindi cha kwanza na mechi ingebadilika kabisa kimbinu. Tulijituma kwa kadili tulivyoweza na tulipata matokeo muhimu.

"Tuliruhusu mabao mawili, kikukweli tunaruhusu mabao mengi zaidi.

"Ulikuwa mchezo mgumu, dimba halikuruhusu kucheza kimbinu zaidi; tulijaribu kushinda hadi dakika ya mwisho, bahati mbaya tulishindwa kufanya hivyo."

Licha ya sare hiyo, Milan bado inaongoza msimamo wa Ligi Kuu na sasa wamewapita wapinzani wao Inter Milan kwa pointi moja tu.

HABARI MICHEZO

# Barca sasa imeamka - Koeman

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anaamini "molari na mtazamo" wa Barcelona katika ushindi wa 2-1 kwenye LaLiga dhidi ya Real Sociedad imethibitisha kwamba wanaweza kurudi katika kiwango chao bora baada ya kuwa na mwanzo mgumu wa msimu huu.

Kocha huyo mkuu wa Barca, Koeman, alisifia kiwango cha timu yake wakati mabao ya Jordi Alba na Frenkie de Jong yaliiwezesha kupata ushindi wa 23 mfululizo kwenye Ligi Kuu ya Hispania dhidi ya Sociedad.

Kikosi hicho cha Koeman kilianza mchezo kwa kutawala, lakini hakikupiga shuti lolote ndani ya dakika 25, wakati Willian Jose alipoiweka mbele Sociedad katika dakika ya 27 pale katika dimba la Camp Nou.

Lakini mabao mawili ndani ya dakika ya 12 yalimfanya Koeman kuondoka akiwa na furaha kwa ushindi huo.

"Kwa molari na mtazamo wa sasa tutakuwa pale tulipostahili kuwapo," alisema Koeman mara baada ya mchezo huo.

"Kwa uhakika kabisa, kipindi cha kwanza kilikuwa bora zaidi kwetu kwa msimu huu. Tulikuwa vizuri kwa kumiliki mpira na kufanya tunachotaka.

"Kipindi cha pili Real ilicheza mchezo mzuri zaidi. Walikuwa na presha kubwa na nguvu kubwa."

Ushindi huo umewanyanyua Barca hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi ikiwa imeshinda mechi sita kati ya 12, ikiwa imepitwa pointi sita na vinara Atletico Madrid, Sociedad na Real Madrid ambao wamelingana pointi kileleni.

Barca mchezo wake unaofuata utakuwa dhidi ya Valencia kesho Jumamosi.






# TUCHEL: BADO NINA IMANI NA ANGEL

**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amesema "kamwe hataacha kumwamini" Angel Di Maria licha ya kwa mara nyingine kumuacha kiungo huyo mshambuliaji nje katika kikosi cha kwanza cha Paris Saint-Germain.

Di Maria amekuwa akiachwa mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza cha PSG na kwa mara nyingine aliwekwa kwenye benchi la wachezaji wa akiba Jumatatu, wakati wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Lorient kwenye Ligi Kuu ya Ufarabsa, Ligue 1.

Raia huyo wa Argentina aliingizwa zikiwa zimesalia dakika 19, wakati bingwa huyo mtetezi tayari alikuwa anaongoza kwa mabao mawili yaliyofungwa na Kylian Mbappe kwa penalti na Moise Kean.

Di Maria aligusa mpira mara 18 wakati wake akiwa dimbani hakuna hata mmoja aliougusa ndani ya eneo la hatari na alishindwa kupiga shuti hata moja.

Na kocha mkuu wa PSG, Tuchel alimuambia Di Maria kuimarika katika uchezaji wake kama anataka kurudi kwenye kikosi cha kwanza mara kwa mara.

"Nahisi kama Angel amepoteza kitu fulani, kitu ambacho ni tofauti kabisa na mwanzo, lakini hivyo ndivyo mambo yalivyo," alisema Tuchel mara baada ya mchezo huo.

"Tulibadilisha mfumo katika dakika za mwisho dhidi ya (RB) Leipzig, kwa Manchester, dhidi ya (Istanbul) Basaksehir hapa na Montpellier.

"Tulikuwa imara zidi kwenye mfumo wa 5-3-2. Inakuwa ni rahisi zaidi kwa Rafinha akiwa kwenye kiungo ya kati, ana uamuzi ya haraka. Lakini hili ni suala la uamuzi kwa sasa."

# Conte asifia kiwango Inter ikishinda

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte alikuwa na furaha wakati Inter Milan ikiibuka na ushindi "mbaya" wa 1-0 dhidi ya Napoli kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, pale kwenye dimba la San Siro, Jumatano.

Kikosi hicho cha kocha, Roberto Gagliardini kilionesha udhaifu kwa kushinda kupiga shuti lolote kipindi cha kwanza, huku Inter wakiongoza kwa bao la penalti la Romelu Lukaku katika dakika ya 73, iliyopatikana kwa David Ospina kumfanyia faulo Matteo Darmian.

Na hilo lilikuwa shuti pekee lililolenga goli kwa Nerazzurri, huku Napoli wakimpoteza nahodha wake, Lorenzo Insigne kwa kutolewa nje kwa kadi nyekundu na mwamuzi, Davide Massa.

"Mchezo ulikuwa mgumu zaidi kimbinu, mchezo ulikuwa mgumu na kila timu ilipambana kutaka kupata matokeo.

"Lakini jambo la msingi ni kwamba tulipata ushindi na pointi tatu zilikuwa muhimu zaidi kwa timu," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.

"Hizi ni mechi ngumu kwa sababu unaweza kushinda na kupoteza pia. Napolini timu ngumu zaidi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: SIKUWA NA FURAHA LIVERPOOL IKIPAA KILELENI

## Asema ni ngumu kucheza na Spurs inashambulia kwa kushtukiza na ndio maana...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema "hakujihisi furaha" baada ya Liverpool kuifunga "kiaina" Tottenham 2-1 na kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England, juzi Jumatano.

**Spurs walionekana kama wataendelea kubakia kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya bao wakielekea kupata sare, lakini bao la Roberto Firmino la dakika ya 90 likawapa ushindi huo kwenye dimba la Anfield na kukaa kileleni kwa tofauti ya pointi tatu.**

Son Heung-min alisawazisha dakika saba baada ya Mohamed Salah kuwapa uongozi wekundu hao, lakini Firmino alimaliza umwamba wa Tottenham wa kutopoteza mechi 11.

Spurs walihisi bao la straika huyo wa Brazil halikupaswa kuhesabiwa kwa sababu Jordan Henderson alimfanyia faulo, Eric Dier kabla ya Firmino kuuwahi mpira wa kichwa wa Andy Robertson.

Steven Bergwijn aligonga mwamba na kukosa nafasi ya kufunga kipindi cha pili, huku Harry Kane akikosa nafasi ya wazi ya kufunga.

Liverpool huo ulikuwa ni ushindi wao wa saba nyumbani kwenye Ligi Kuu, huku Sadio Mane akigonga mwamba wakati Liverpool ilipopiga mashuti 17 na 11 kati yake yakilenga goli na Tottenham wakipiga mashuti nane.

Mara baada ya mchezo huo Klopp aliwaambia waandishi wa habari: "Kucheza soka kama hili usiku huu kwa hakika kabisa ni jambo la aina yake.

"Tulistahili pointi tatu dhidi ya kikosi cha juu. Ni ngumu sana kucheza dhidi yao ambapo walikuwa wanacheza kwa staili ya mashambulizi ya kushitukiza..

"Kwa uhakika nafikiri tulistahili pointi tatu. Najua kwamba walikuwa na nafasi, na ndio maana walifunga bao."

## ZISIKUPITE

### JUVE WAZUNGUMZA NA POGBA

JUVENTUS imefungua mazungumzo na wakala wa Paul Pogba, Mino Raiola wakati wakitaka kumsajili tena kiungo huyo wa Manchester United mwenye umri wa miaka 27. ***(Express)***

### TOMORI HUYO RENNES

MLINZI wa Chelsea na England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Leeds United, anapanga kujiunga na klabu ya Ufaransa ya Rennes kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu. ***(Talksport)***

### LIVERPOOL YAMTAKA SANCHEZ

LIVERPOOL inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Ureno na Lille, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 23. ***(Le10 Sport)***

### WILLIAMS KUACHIWA JANUARI

MANCHESTER United itasubiri hadi Januari kuamua kama mlinzi wa kushoto, Brandon Williams, mwenye umri wa miaka 20 anayehusishwa na Southampton na Newcastle - ataondoka kwa mkopo. ***(Manchester Evening News)***

### GIROUD KUBAKI CHELSEA

CHELSEA inajiamini kwamba inaweza kumbabikisha Olivier Giroud wakati wa dirisha dogo la Januari na kuendelea kumpa nafasi straika huyo mwenye umri wa miaka 34. ***(Telegraph)***

### MAN U NA USAJILI

KLABU ya Manchester United bado ipo zokoni kutafuta winga, mlinzi wa kati na kulia na kiungo mkabaji, lakini matarajio ni kwamba hakutakuwa na usajili dirisha dogo la Januari. ***(Manchester Evening News)***

### NEYMAR HARUDI BARCA

FOWADI wa Paris St-Germain, Neymar amekanusha uvumi kwamba anatarajia kurudi Barcelona, ambapo nyota huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 28 amesisitiza ana furaha pale kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa. ***(Express)***

### ARSENAL YAMUWANIA VIEIRA

ARSENAL inaweza kufanya usajili Januari kwa kumchukua kiungo wa Porto, Fabio Vieira na wapo tayari kulipa pauni milioni 27 kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Record, via Mail)***

### MAN U YARUDI KWA NIGUEZ

KLABU ya Manchester United imefufua nia yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez, mwenye umri wa miaka 26. ***(Todo Fichajes, via Team Talk)***

### ISCO AWANIWA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amewataka mabosi wake kumsajili kiungo wa Real Madrid na Hispania, Isco, 28, na kiungo wa Ufaransa na Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22 wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Defensa Central, via Team Talk)***

## HABARI MICHEZO

### Kocha KMKM afurahia ushindi mfululizo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya KMKM, Ame Msimu, amesema kupata ushindi mfululizo wa mechi mbili kumetokana na kufanyia kazi upungufu ambao ulikuwa ukijitokeza mara kwa mara kwa wachezaji wake.

Alisema miongoni mwa mambo aliyoyafanyia kazi ni kuhakikisha wachezaji wanazidisha umakini pindi wawapo golini na kuzitumia vizuri nafasi wanazozipata ili timu ifunge mabao.

KMKM ilipaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidhi ya timu ya Kipanga, juzi Jumatano.

Ushindi huo uliwafanya KMKM kufikisha alama 12 kwenye ligi hiyo na kukaa kileleni mwa msimamo.

Msimu alisema kwa sasa anachotaka ni kuhakikisha timu yake inashinda mechi zake zote za nyumbani.

Mabao ya KMKM yalifungwa na Ilyasa Suleiman Mohamed dakika ya 5 na Matheo Antony dakika ya 64.

### Azam kumaliza ukame wa ushindi leo?

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Azam FC, leo saa moja usiku itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Azam Complex, kucheza na Ruvu Shooting katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hiyo ni mechi ya raundi ya 15, na Azam itaingia uwanjani ikiwa ni mechi ya pili kwa kocha George Lwandamina aliyechukua mikoba ya Aristica Cioaba, ambaye alifukuzwa baada ya kuchapwa bao 1-0 na Yanga Novemba 25, mwaka huu.

Azam, inayoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu hadi sasa ikiwa na pointi 28, itaingia uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya 2-2 Namungo kwenye mchezo uliopita.

Timu hiyo inahitaji ushindi kwa udi na uvumba ili kurejesha imani kwa mashabiki wake ambao hawajashuhudia ikishindi tangu Novemba 5 mwaka huu, wakati ilipoichapa Dodoma Jiji mabao 3-0.

Baada ya mchezo huo, imecheza mechi tano bila kupata ushindi, ikifungwa bao 1-0 na KMC, ikachapwa 1-0 na Yanga, suluhu mbili dhidi ya Biashara na Gwambina, kabla ya sare ya bao 2-2 na Namungo.

# MWAMUZI ALIKOSEA KIBINADAMU - KASEJA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa KMC, Juma Kaseja, amesema kuwa makosa aliyoyafanya mwamuzi ni ya kibinadamu na wala hayakuwa na nia mbaya au kufanya makusudi.

**Akizungumza baada ya mechi kati timu yake dhidi ya Simba ambapo walifungwa bao 1-0 juzi Jumatano, Kaseja alisema kuwa soka siku zote ndivyo lilivyo na mwamuzi ni binadamu kama ambavyo yoyote hukosea.**

"Mechi ilikuwa nzuri na ya ushindani, tulivyocheza ndivyo tulivyojiandaa na kuhusu ile penalti, unajua mwamuzi naye ni binadamu, sisi tuliona siyo penalti, lakini yeye aliona ni penalti. Basi ndiyo hivyo, alikosea kibinadamu tu," alisema Kaseja ambaye alifanya kazi kubwa kwenye mechi hiyo.

Hata hivyo, alisema kuwa waamuzi kwenye Ligi Kuu wanatakiwa kuwa makini wanapochezesha mechi, kwani wanapofanya kosa, linagharimu timu ambayo imekuwa ikijiandaa kukaa kambini kwa gharama na kulipa wachezaji posho.

"Yote kwa yote, nasema mwamuzi ni binadamu, tuchukulie upungufu ni wa kibinadamu na si makusudi kama ambayo mchezaji anaweza kufanya kosa uwanjani kukosa goli, au kufungisha, mechi imeisha kila timu ijiandae na mechi inayofuata," alisema.

Kwenye mechi hiyo iliyochezeshwa na mwamuzi Elly Sasi, Simba ilipata bao dakika ya 76 likifungwa na Meddie Kagere kwa mkwaju wa penalti ambayo ililalamikiwa sana na baadhi ya mashabiki kwa madai kuwa mchezaji, Hassan Kabunda hakuunawa mpira.

Kwa matokeo hayo KMC sasa inakamata nafasi ya tano ikiwa imesalia na pointi zake 21 kwa mechi 14 ambazo imecheza, huku wapinzani wao Simba wakiendelea kujishindilia kwenye nafasi ya pili kwa pointi 32, ikicheza mechi 14 mpaka sasa.



Msanii Banana Zoro akiimba wimbo maalum wa Serebuka pamoja na kundi lake, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Serebuka mapema mwaka huu, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kampeni ya Serebuka yamalizika kwa kumwaga zawadi*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI ya Serebuka inayoendeshwa na kampuni ya Serengeti kupitia bia zake za Serengeti Lager na Serengeti Lite, imemalizika kwa kuwajaza Watanzania zawadi na fedha taslimmu katika msimu huu wa sikukuu na kuwaacha wakiwa na furaha kubwa.

Kampeni hiyo ya Serebuka ililenga kuwahamasisha Watanzania na watumiaji wa bia ya Serengeti Lager na Serengeti Lite kufurahia maisha bila kikomo.

Mkuu wa kitengo cha bia wa Serengeti, Anitha Msangi, amesema kampeni ya Serebuka ilimlenga kila Mtanzania huku ikimpa nafasi ya kufurahia maisha kupitia muziki, chakula na kinywaji bora cha bia ya chapa Serengeti.

Pamoja na muziki, chakula na vinywaji, Watanzania pia waliweza kupata burudani za kupitia vichekesho na michezo mbalimbali, huku nyota wenye majina makubwa katika tasnia mbalimbali wakihusika kuipa nguvu.

"Tumekuwa na changamoto au mashindano ya aina mbalimbali yaliyowahusisha mastaa ambao waliwaburudisha Watanzania katika kipindi cha kampeni hii," alisema Anitha wakati wa kukabidhi zawadi za fedha taslimu kwa baadhi ya washindi wa kampeni jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.

Baadhi ya washindi waliomaliza mwaka vizuri ni pamoja na Dbaba Tz's kutoka mkoani Mwanza, Grace Mella na Juma Omary wote wakazi wa Dar es Salaam, ambapo kila mmoja alijishindia fedha taslimu, shilingi milioni moja baada ya kupigiwa kura nyingi na kuibuka washindi katika shindano la kuimba, kucheza na kuchekesha.

Akizungumza baada ya kupokea zawadi yake, Grace Mella alisema fedha hiyo itamfanya afurahie msimu wa sikukuu vizuri zaidi na kuwataka Watanzania kutumia bidhaa bora za Serengeti ambazo pia zinatoa fursa mbalimbali kwa wateja wake kama ilivyotokea kwake.

Juma Omari ambaye ni mshindi mwingine wa shilingi milioni moja, alisema kupitia shindano la kuchekesha limeweza kumpa nafasi ya kuonyesha kipaji na tayari ameshaanza kupata washirika wa kufanya naye kazi kupitia sanaa ya vichekesho.

# Michezo

Ijumaa Desemba 18, 2020

Nipashe




Klopp: Sikuwa na furaha Liver ikipaa kileleni UKURASA 22



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya wenye ulemavu 'Tembo Warriors', wakijifua kwenye mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SVEN AKUNWA NA KMC, AIFUNGIA KAZI PLATINUM

## ●●● Amesema anachofurahi na kuwapongeza wachezaji katika mechi hiyo ni kupata pointi tatu bila ya...

**Na Saada Akida**

BAADA ya juzi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC FC, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amewasifu wapinzani wao kwa kuonyesha kiwango kizuri na sasa wanajipanga kuwavaa FC Platinum ya Zimbabwe.

**Simba imepaa leo Ijumaa kuelekea nchini Zimbabwe kwa ajili ya kuwavaa Platinum kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika, utakaopigwa Jumatano ijayo ya Desemba 23.**

Simba itacheza na timu hiyo ya Zimbabwe, baada ya kupenya hatua ya awali kwa kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa ushindi wa bao 1-0 walilolipata kwenye mchezo wa ugenini, kabla ya kulazimishwa suluhu kwenye mchezo wa pili uliopigwa dimba la Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Sven alisema mchezo wao dhidi ya KMC ulikuwa wa ushindani mkubwa ambao umekuwa kipimo kikubwa cha kuona upungufu wao kabla ya kuwavaa Platinum.

Alisema anachofurahi na kuwapongeza wachezaji wake katika mechi hiyo ni kupata pointi tatu bila ya kujali ni aina gani ya bao ambalo wamefunga, kwa sababu matokeo ya uwanjani huamuliwa na mwamuzi na dakika 90 za mchezo.

"Hii mechi imeshapita, sasa tunaangalia mbele zaidi kufanyia kazi upungufu wetu kwa sababu kuna majukumu makubwa mbele yetu, kuwakilisha nchi katika michuano ya kimataifa, kucheza dhidi ya Platinum ambayo tunaenda ugenini."

"Hautakuwa mchezo mwepesi, tunakwenda kupambana ili kufanya vizuri, hii ni Ligi ya Mabingwa Afrika huku kuna ushindani mkubwa tofauti na ligi," alisema Sven.

Alisema baada ya tathmini ya mchezo wao dhidi ya KMC, watajua wachezaji ambao wataenda nchini Zimbabwe kukabiliana na wenyeji wao hao kuhakikisha wanapata matokeo chanya ugenini.

Sven alisema kulingana na maisha ya mchezaji nje ya kambi haoni kuna shida kauli na kitendo cha kuwaonyesha (kidole cha kati) nyota wake, Bernard Morrison na kusisitiza kauli aliyotoa ni sawa ila kitendo cha hiko kidole ndio amekosea.

"Hayo ni maisha ya mchezaji nje ya klabu, alichokiongea ni sawa ila kitendo alichokifanya kimeleta shida," alisema kocha huyo.

Naye beki wa Simba, Shomari Kapombe alisema baada ya kupata pointi tatu dhidi ya KMC sasa wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mechi yao dhidi ya FC Platinum ana amini kwamba utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu kuna baadhi ya nyota waliwahi kucheza soka Tanzania.

"Itakuwa mechi ngumu kwa sababu kuna baadhi ya wachezaji ambao wamewahi kupita na kucheza soka hapa nchini akiwamo Thaban Kamusoko na Elius Maguli ambaye naye aliwahi kucheza Simba," alisema Kapombe.

Alisema mashabiki waendelee kusapoti katika kila mechi na kuwahakikishia wanaenda Zimbabwe kupambana kutafuta matokeo mazuri na ikiwezekana kumaliza kazi ugenini kabla ya kurejea nyumbani katika mchezo wa marudiano.

Simba watacheza mchezo wa kwanza ugenini unaotarajiwa kuchezwa Desemba 23 na ule wa marudio unatarajiwa kuchezwa Uwanja wa Mkapa Januari 6.

# Kaze: Hatuna mzaha kwa Dodoma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mechi ya kirafiki dhidi ya Singida United, imempa mwanga wa kuona upungufu wake, huku akisisitiza pointi tatu ni muhimu katika mechi yao ya kesho Jumamosi dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaze alisema kwa muda mfupi aliokaa nchini ameona ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu, na hivyo anaendelea kuwapa mbinu zaidi washambuliaji wake kuhakikisha wanashinda kila mchezo.

Alisema ana imani ligi bado ndefu, wanalazimika kuwa makini na kutorudia makosa ambayo yanajitokeza katika mechi za nyuma, ikiwamo suala la kutumia vema nafasi wanazotengeneza na umakini katika safu ya ulinzi na ushambuliaji.

"Ligi ina ushindani mkubwa, hatutadharau timu yoyote tutakayokutana nayo, hivyo tunaenda kucheza na Dodoma ambao sio wabaya wana kikosi kizuri na wamejipanga kutafuta pointi tatu, hata sisi tunahitaji kupata pointi tatu ili kufikia malengo yetu," alisema Kaze.

Wakati huo huo, Kaze amesema kwamba ameshapendekeza nafasi tatu ya wachezaji ambao wanahitajika kusajiliwa katika dirisha hilo dogo.

Amesema safu ya ushambuliaji imechukuliwa na Saido Ntibanzokiza na atacheza dhidi ya Dodoma na itakuwa mechi yake ya kwanza katika Ligi Kuu baada ya kuanza kucheza kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Singida na kufunga mabao mawili.

Kocha huyo alisema pia kuna kiungo mshambuliaji pamoja na beki, jambo ambalo linahitaji kukaa na kufikiria zaidi katika usajili huo kupata wachezaji ambao watabadilisha matokeo.

"Hutakiwi kusajili kutokana na presha za mashabiki au viongozi, tunahitaji wachezaji ambao watasaidia timu kufikia malengo yetu, kama nilivyoeleza awali kwamba tunahitaji kupata watu ambao watatusaidia katika malengo yetu," alisema Kaze.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042